SportPesa
TZS. 761,374,640
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



**TIPER** yataja dawa kumaliza upandaji wa bei za mafuta

UKURASA 2



**Pele alazwa tena hospitalini**

UKURASA 22


# Nipashe

Ijumaa Desemba 10, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580790

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


## MIAKA 60 YA UHURU

# Ilivyotia fora


UKURASA 2





Rais Samia Suluhu Hassan, akipunga mkono kwa wananchi wakati akiwasili kwa gari maalum la Jeshi la Ulinzi wa Wananchi wa Tanzania (JWTZ), katika Uwanja wa Uhuru, mkoani Dar es Salaam jana, kwa ajili ya sherehe za maadhimisho ya Miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara. **Picha nyingine:** Maonyesho mbalimbali ya vikosi vya ulinzi. Kulia kwa Rais ni Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali Venance Mabeyo. **Picha zaidi Uk. 19. PICHA: IKULU**











MICHEZO NABI AWAPA WALINZI MAJUKUMU YANGA UK.24 MAONI, KATUNI UK.6

# TIPER yataja dawa udhibiti bei mafuta

**Na Romana Mallya**

KAMPUNI ya Uhifadhi Mafuta (TIPER), imesema endapo maghala yake yatatumika kupokea mafuta yote yanayoingia nchini, muda wa meli wa kupakua bidhaa hiyo utapungua na hatimaye kupungua gharama za meli ambazo zina mchango mkubwa katika utoaji wa bei sokoni.

Naibu Mkurugenzi Mtendaji TIPER, Martin Mosha, aliyasema hayo juzi katika mkutano wake na wahariri na waandishi wa habari uliofanyika katika ofisi za kampuni hiyo, Kigamboni mkoani Dar es Salaam.

"Matumizi ya miundombinu ya TIPER kuhifadhi mafuta yanayoingia ni njia nzuri ya serikali na taasisi zake, wakiwamo wadau wa mafuta kusaidia kupunguza muda wa meli wa kupakua, hivyo kupunguza gharama za meli. Hatua hii pia itapunguza hata bei za mafuta nchini," alisema.

Pia alisema kazi hiyo ya kushusha mafuta kwenye meli ikifanywa sehemu moja, itapunguza siku kutoka 10 hadi sita na itakuwa rahisi kuthibiti kodi.

Mosha alisema TIPER kwa ukubwa wake inaweza kusaidia kupunguza bei ya mafuta au kuithibiti endapo yatashushwa katika maghala ya kampuni hiyo.

"Inakuaje? Mafuta katika soko la dunia huwa yanapanda na kuna wakati yanashuka bei, kwa hiyo waagizaji kuna wakati wanapata kwa bei ya chini na kuna wakati bei ya juu kama ilivyo sasa.

"Kama una hifadhi kubwa ya mafuta kama tulivyosema unakuwa na lita milioni 300 ambazo uliziagiza ukaweka TIPER kwa asilimia 30 ya bei ya sasa ambazo ndiyo bei zinazokwenda maana yake bei zinapopanda unakuwa na mafuta ya bei ile.

Unaweza kutumia na yasipande kwa kiwango ambacho kimepanda katika soko la dunia," alisema Mosha huku akibainisha kuwa hiyo ni faida ya kuwa na hifadhi kubwa ya kimkakati ya petroli kama waliyo nayo.

"TIPER tunatamani kujiendesha kama 'bonded warehouse'. Kodi inalipiwa tu wakati unapochukua na kuanza kuyatumia yanakuwa hayana kodi.

Hata watu wanaotaka kuyapeleka 'transit' (kwenda nje) yakiwa hapa mfano wanataka soko la Jamhuri ya Demokrasia ya Congo (DRC) akilipata ndiyo anakuja kuchukua," alisisitiza.

Mosha alisema hatua hiyo inasaidia mafuta yanapokuwa kwenye soko wanaweza kuuza kwa bei ndogo kuliko inayokuwapo wakati huo.

Aidha, alisema kuanzia mwaka 1999 kampuni hiyo imekuwa inajenga uwezo wake ili kuwa na ufanisi katika kuhudumia na kupokea mafuta katika meli, kuhifadhi na kuyatoa katika maghala yao hadi sehemu mafuta hayo yanaweza kuchukuliwa. Alisema wanatekeleza jukumu hilo katika Bandari ya Dar es Salaam kwenye eneo lenye ukubwa wa hekta 58 (ekari 143).

"Ukubwa huu unaipa sifa kampuni yetu kuwa sehemu ya maghala mengi yenye hifadhi ya mafuta mengi kwa mara moja. Tuna jumla ya maghala 33 ambapo 32 kati yake ndiyo yanayotumika. Maghala 11 yenye mita za ujazo 180,000 kwa ajili ya dizeli, maghala 16 yenye mita za ujazo 56,000 za petroli, maghala mawili yenye mita za ujazo 6,000 kwa ajili ya mafuta ya taa na maghala matatu yenye mita za ujazo 11,000 kwa ajili ya mafuta mazito ya mitambo, hivyo kufanya jumla ya mita za ujazo wa mafuta ya TIPER kuwa 253,000."

Mosha alisema maghala yote yamefungwa vifaa vya kieletroniki ambavyo vinatumika kutambua ujazo wa mafuta yaliyo katika maghala hayo na wana jumla ya mita sita (flow meters).

Kuhusu mradi wa ujenzi wa bomba la mafuta linalojengwa kutoka Hoima, Uganda hadi Tanga, Tanzania, Mosha alisema kampuni yao tayari ina ardhi Tanga hivyo watajenga matangi ya kuhifadhi mafuta huko.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Mwinyi akikabidhi kikombe cha pongezi kwa Mkuu wa Fedha wa TBL, Avito Swai kwa niaba ya kampuni, baada ya kuwa mshindi wa kwanza kwa kuchangia kulipa kodi, katika hafla ya taasisi zilizotoa mchango kukuza uchumi katika maadhimisho ya miaka 60 ya Uhuru, jijini Zanzibar mapema wiki hii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Miaka 60 ilivyotia fora

**Na Waandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan ameongoza sherehe ya maadhimisho ya miaka 60 ya uhuru wa Tanzania Bara zilizotia fora kwenye Uwanja wa Uhuru mkoani Dar es Salaam jana.

Sherehe hiyo ya maadhimisho ya siku ya uhuru wa nchi ilihudhuriwa na marais kutoka nchi jirani na maelfu ya Watanzania, ikiwa ni ya kwanza kwa Rais Samia tangu aapishwe kushika nafasi hiyo Machi 19 mwaka huu baada ya kifo cha Dk. John Magufuli Machi 17 mwaka huu.

Baada ya kuwasili uwanjani huko, Rais Samia alikagua gwaride maalumu lililoandaliwa kwa ajili ya siku hiyo muhimu.

Marais waliohudhuria sherehe hizo ni: Uhuru Kenyatta wa Kenya ambaye pia ni Mwenyekiti wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Paul Kagame wa Rwanda, Filipe Nyusi wa Msumbiji, Othman Ghazali wa Visiwa vya Comoro ambaye pia ni Makamu Mwenyeti wa Pili wa Umoja wa Afrika (AU).

Viongozi wengine waliokuwapo kwenye Uwanja wa Uhuru jana ni Rais mstaafu wa Malawi Joyce Banda na Rais mstaafu wa Msumbiji, Joackim Chissano.

Wengine ni Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Jean-Michel Lukonde na Makamu wa Rais wa Burundi, Prosper Bazombanza.

Pia kulikuwa na wajumbe maalumu waliowawakilisha marais na wakuu wa nchi za Botswana, Uganda, Afrika Kusini, Zimbabwe, Oman na Eswatin.

Mbali na wageni hao, sherehe hiyo pia ilihudhuriwa na marais wastaafu wa Tanzania, mabalozi, wabunge na wawakilishi wa jumuiya za wafanyabiashara.

Kwenye sherehe hizo zilikuwapo burudani mbalimbali ikiwamo ngoma za asili kutoka makabila na maeneo tofauti nchini, wasanii na halaiki ya wanafunzi wa shule za msingi.

Rais Samia aliwashukuru wageni na wananchi wote waliohudhuria sherehe hiyo.

**ILIVYOTIA FORA**

Katika sherehe hiyo wananchi na viongozi waliohudhuria walipata fursa kuona shughuli mbalimbali za Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) na kivutio kikubwa kilikuwa ni halaiki ya wanafunzi zaidi ya 600 waliotengeneza maumbo yenye ujumbe tofauti.

Pia gwaride la vikosi vya ulinzi na usalama vilitia fora huku Jeshi la Uhamiaji likishiriki kwa mara ya kwanza baada ya kuanzishwa kwake kisheria miezi miwili iliyopita.

Baada ya viongozi waalikwa kuwasili uwanjani hapo, Rais Samia akiwa kwenye gari maalumu la jeshi, aliingia na kuzunguka uwanja kusalimia maelfu ya wananchi waliojitokeza.

Wimbo wa Taifa na Wimbo wa Afrika Mashariki ziliimbwa kisha mizinga 21 kupigwa na baadaye alikwenda kukagua gwaride rasmi lililoandaliwa kuadhimisha miaka 60 ya uhuru.

Baadaye kulikuwa na maonesho maalumu la makomandoo wa JWTZ walioshuka kwenye chopa kwa kamba kisha watoto wa halaiki wakahitimisha burudani kwa kuchora maumbo mbalimbali yaliyoonekana kuvutia waliohudhuria.

Katika hatua nyingine, jana jioni Rais Samia aliwatunuku nishani maalumu ya miaka 60 ya uhuru Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Mkuu wa Jeshi la Polisi, Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na Kamishna Jenerali wa Jeshi la Uhamiaji.

■**Imeandikwa na Romana Mallya na Christina Mwakangale.**


**KUPOTELEWA NA KADI YA GARI**

**DAVID CONSTANTINO HAULE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari iliyokuwa na namba ya usajili **T 743 DSC** Toyota Harrier yenye chasis namba **ACU350008494** na engine namba **2AZ1688922**. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

**Taarifa ya Polisi: IRI/IRI/RB/578209/2021**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA TANZANIA**

**Katika mahakama ya Mwanzo kihonda Wilaya ya morogoro**

**Mkoa wa morogoro**

**Usimamizi wa Mirathi Na……06..2021**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU PETRO MAJIRA TLATLA WA KIHONDA MOROGORO**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA KORNEL MAJIRA TLATLA.**

**TANGAZO**

**(Kanuni ya 5(2)ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhulia katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 10/12/2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Zingatia;

Endapo kuna yoyote mwenye wosia wa marehem anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

- Wosia wa marehem huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa.
- Marehem hakuacha wosia
- Futa isiyohusika

Imetolewa leo tarehe 07 mwezi 12 Mwaka2021

HAKIMU MAHAKAMA YA MWANZO KIHONDA MOROGORO

**THE REGISTRATION OF DOCUMENTS**
**CAP. 117**

**DEED POLL ON CHANGE OF NAME**

BY THIS DEED, I the undersigned **MAGRETH MARIO KAONEKA** Phone-0713951717 Tanga. Do hereby absolutely renounce and abandon the use of my former names of **MAGRETH KIMARIO KAONEKA** and **MAGDALENA MARIO KAONEKA** and in lieu thereof do assume from the date hereof the name of **MAGRETH MARIO KAONEKA.**

**AND**

That the name **MAGRETH KIMARIO KAONEKA** is from my National Identification Card No: 19860529-21201-00001-10 and **MAGDALENA MARIO KAONEKA** is from my Marriage Certificate NO. 0455245 and **MAGRETH MARIO KAONEKA** is from Voter Card No. T-1000-9436-490-0, they all refers to one person namely **MAGRETH MARIO KAONEKA.**

**AND**

I hereby declare that I will be known at all times hereafter in all records, deed and instrument in writing and in all actions and whatsoever use and sign the said name of MAGRETH MARIO KAONEKA.

**AND**

And I do hereby authorize and request all persons to describe and address me by such assumed name of MAGRETH MARIO KAONEKA.

BEFORE ME:
NAME: ……
SIGNATURE: ……
ADDRESS: ……
OCCUPATION: ……

HAKIMU MKAZI MAHAKAMA YA MWANZO TANGA MJINI

## RIPOTI MAALUM

# Neema ya mgodi inapogeuka shubiri

**Na Mwandishi Wetu,** TARIME

UNAPOKANYAGA Kitongoji cha Kigonga B kilichoko Kijiji cha Matongo, Kata ya Matongo wilayani Tarime, unashuhudia nyumba za wakazi wake zikiwa zimebomolewa isipokuwa makazi ya Sadock Maningo (pichani).

Mahali hapo ni umbali wa Km 85 kusini mashariki mwa Mji wa Tarime na safari yake kutoka mjini Tarime inachukua takriban saa moja na dakika 35 kwa gari ukipita Barabara ya Nyamongo ambayo ni ya vumbi.

Kwenye kitongoji hicho nyumba zimebomolewa ili kupisha upanuzi wa mgodi wa dhahabu wa Nyamongo, lakini Manongi amekataa kupokea Sh. milioni 62.905 zilizopendekezwa kulipwa kwake kama fidia ya ardhi, mali na usumbufu.

Ni saa nne asubuhi, Nipashe inazuru kwenye makazi ya baba huyo wa watoto sita (watatu wa kike) yaliyoko takriban mita 300 kutoka kwenye mgodi huo wa dhahabu.

Akizungumza kwa utulivu na kujiamini huku akionyesha baadhi ya nyaraka za tathmini ya mali zake, Maningo (48) anasimulia:

"Kama unavyoona hapa kwenye kitongoji chetu hiki yamebaki makazi yangu tu, wenzangu wamelipwa fidia na kuondoka. Mimi nimelazimika kubaki kwa sababu ninaona wazi kabisa fedha ninazolipwa haziakisi thamani ya ardhi na mali zilizopo hapa.

"Tazama nina nyumba hizi kubwa mbili na hizo ndogo ndogo tatu, ardhi hii na vilivyomo sidhani kama thamani yake ni shilingi milioni 62."

Maningo ambaye kielimu aliishia darasa la saba, anaendelea kusimulia kiini cha mvutano wake na wamiliki wa mgodi huo, akirejea nyaraka za uthibitisho wa malipo ya fidia, akitamka:

"Kama unavyoona hapa kwenye nyaraka, tathmini ya kwanza ilifanyika Septemba 26 mwaka juzi (2019). Wakasema mali zangu zote hapa zina thamani ya Sh. milioni 129 (takwimu halisi zilizopo kwenye nyaraka ni Sh. 129,354,560).

"Nilikubali kulipwa kiasi hiki cha fedha maana walau kilikuwa kinaakisi thamani ya mali zangu, lakini cha kushangaza nilipokwenda Ofisi ya Uhusiano (ya Kampuni ya Barrick North Mara) nilikuta malipo yangu ni Sh. milioni 62 (takwimu halisi Sh. 62,905,384.72).

"Nilishtuka sana, nikakataa kabisa kusaini hizi nyaraka za malipo. Tathmini ya pili ilifanyika Mei 11 mwaka huu (2021). Wamesema eneo langu na vilivyomo thamani yake ni Sh. milioni 83 (takwimu halisi Sh. 83,716,994).

"Nimekataa pia kusaini malipo haya kwa sababu ninaona ninapunjwa. Ninataka wanilipe kulingana na tathmini ya mwanzo kabisa (Sh. milioni 129).

"Nipo hapa tangu mwaka 1994, eneo hili nilipewa na baba yangu mzazi. Ninatambua kuishi karibu na mgodi wa madini ni hatari lakini siwezi kukubali kuliachia eneo hili (lina ukubwa ekari 1.386) kwa malipo hayo wanayotaka wao. Vifaa vya ujenzi vimepanda bei. Nitawezaje kujenga tena nyumba zote hizi kwa Sh. milioni 83."

Wakati hali ikiwa hivyo kwa Maningo, kwenye Kitongoji cha Nyamichere, Kijiji cha Nyakunguru, wakazi wake wamesubiri fidia ya kupisha upanuzi wa mgodi huo wa dhahabu kwa miaka tisa sasa.

Peter Chacha, mmoja wa wakazi wa eneo hilo, anasema walizuiwa kuendeleza maeneo yao tangu mwaka 2012 na kwamba tathmini ya kwanza ilifanyika mwaka uliofuata, yaani 2013.

Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Timus Chacha, anabainisha kuwa familia 1,900 zimeathiriwa na kuchelewa huko kwa fidia hiyo, akikumbusha kuwa mpaka sasa tayari kumeshafanyika tathmini ya maeneo yao mara tatu.

"Maeneo yote yaliyofanyiwa uhakiki tumezuiwa kufanya shughuli za maeneo. Miaka tisa sasa hatufanyi chochote kwenye maeneo yetu na hatujui hatima ya fidia yetu," anasema.

***ITAENDELEA KESHO**




## MAMLAKA YA DAWA NA VIFAA TIBA

TMDA
Tanzania Medicines & Medical Devices Authority

### MIAKA 60 YA MAFANIKIO KATIBA UDHIBITI WA DAWA NCHINI



1. Kufikia Ngazi ya Tatu ya WHO ya ubora wa mifumo ya udhibiti ( Maturity Level 3) na kuiweka Tanzania kuwa nchi ya kwanza Africa kufikia hatua hiyo
2. Kupata na kushikilia Cheti cha Ithibati cha ISO 9001:2015
3. Kusajili Zaidi ya bidhaa 16,467 dawa baada ya kujiridhisha na ubora, usalama na ufanisi wake hivyo kuongeza wigo wa upatikanaji wa bidhaa na kulinda afya za wananchi
4. Kusogeza huduma kwa wananchi kwa kujenga ofisi za kanda na maabara ya kisasa na kuweka mitambo yenye uwezo za kupima kwa ufanisi usalama na ubora wa bidhaa
5. Kuongeza bajeti kulikowezesha utoaji huduma kwa ufanisi na kutoa gawio kwa serikali kila mwaka hadi kufikia Tsh billion 41.2
6. Kutoa msaada wa kiufundi kwa ajili ya kuanzishwa viwanda vya dawa vipya 15 nchini na vifaa tiba hivyo kuchangia katika uwekezaji nchini
7. Kuanza kutumia mifumo ya kielektroniki katika utoaji huduma za vibali ambapo sasa vinatolewa ndani ya saa 24

1961-2021

MIAKA 60 YA UHURU;
Tanzania Imara, Kazi iendelee.

Imetolewa na:
Mkurungezi Mkuu,
Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba(TMDA),
S.L.P 77150,Dar es Salaam au
S.L.P 1253 Dodoma
Simu:+255 222 450512/450751/452108
Simu ya Bure: 0800110084
Nakushi:+255 222 450793

"TMDA Hulinda Afya ya Jamii"

0800110084 @tmda_tanzania @tmda tanzania www.tmda.go.tz

HABARI KITAIFA

# Madini yanayotumika kutengeneza magari ya umeme yagundulika nchini

**Na Thobias Mwanakatwe**

MADINI aina ya rare earth yanayotumika kutengeneza magari ya umeme na sumaku, yamegundulika katika kata ya Ngwala wilayani Songwe.

Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Omary Mgumba, alitangaza kugundulika kwa madini hayo juzi wakati wa maadhimisho ya miaka 60 ya Uhuru wa Tanganyika yaliyofanyika katika kata ya Nambizo.

Kugundulika kwa madini hayo, alisema kutaifanya Tanzania kuwa nchi ya tatu kuwa nayo baada ya Marekani na China.

Mgumba alisema Desemba 13, mwaka huu, kampuni ya Peak Resources kutoka Australia itapewa leseni ya kuanza kazi, hafla ambayo itafanyika Dodoma.

Alisema kampuni hiyo itakapopata leseni itaanza ujenzi wa miundombinu kwenye mgodi kwa gharama ya Sh. milioni 200 na kwamba ajira 3,600 zitapatikana.

Mkuu wa Mkoa alisema mgodi huo utakapoanza kazi utaajiri wafanyakazi 550 wakiwamo wa muda 300 na gharama za uendeshaji wa mradi zitakuwa Dola za Marekani milioni 37 (sawa na Sh. bilioni 88.8).

Mgumba alisema ukianza uzalishaji utakuwa na manufaa makubwa kiuchumi kwa taifa na kwamba ni muhimu wananchi wakaendelea kushirikiana na wawekezaji.



Mkurugenzi wa Masoko na Mauzo Coca-Cola Kwanza Tanzania, Josephine Msalilwa (kushoto), akifurahia jambo na Meneja wa Masoko ya Biashara wa kampuni hiyo, Wahda Mbaraka, baada ya uzinduzi wa kampeni ya 'Maajabu Halisi na Coca Cola", jijini Mbeya mapema wiki hii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**


**EAST AFRICA STEEL TOWER CO. LIMITED**

**S.L.P 34359 DAR ES SALAAM**

**NAMBA YA USAJILI: 128437**

**TAARIFA YA KUFUNGA KAMPUNI KWA HIARI**

**(Chini ya Kifungu cha 334(1) cha Sheria ya Makampuni Na. 12 ya 2002)**

Inatolewa taarifa kwa Umma kwamba mnamo tarehe 26 mwezi Novemba, 2021 kampuni ya **EAST AFRICA STEEL TOWER CO. LIMITED** ilifikia uamuzi wa kuifunga kwa hiari.

Taarifa inatolewa kwamba **BENO KINYAMAGOHA** ameteuliwa kuwa Mfilisi wa kampuni.

Wadau wote wa Kampuni hii mnaombwa kutoa taarifa za kina juu ya madai yenu katika anwani iliyotolewa hapo chini ndani ya siku kumi na nne (14) baada ya kuchapishwa Tangazo hili.

**Imetolewa Dar es Salaam leo tarehe 26 mwezi Novemba, 2021.**

**BENO KINYAMAGOHA, (MFILISI)**
**S.L.P. 34359 - DAR ES SALAAM**
**Sam Nujoma road, Lufungila street**
**SIMU: +255753614256**
**EMAIL: bennoausebio@gmail.com**


# Balozi Mulamula asema kuna kazi kubwa kumaliza ukatili wa kijinsia

**Na Jenifer Gilla**

WAZIRI wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Liberata Mulamula (pichani), amesema ingawa Tanzania imepiga hatua kupambana na ukatili wa kijinsia, bado kuna kazi kubwa ya kufanya ili kumaliza tatizo hilo.

Aliyasema hayo katika kongamano la kuadhimisha siku 16 za unyanyasaji wa kijinsia liliiloandaliwa na Shirika la Maendeleo ya Ujerumani (GIZ) kwa kushirikiana na Serikali ya Tanzania na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) lenye kaulimbiu 'Ushirikiano Usio na Mipaka Dhidi ya Ukatili wa Kijinsia' lililofanyika katika ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Mwalimu Nyerere, jijini Dar es Salaam.

"Unyanyasaji wa kimwili na kingono dhidi ya wanawake bado umekithiri na mbaya zaidi wahusika wengi wa unyanyasaji wa majumbani hawaadhibiwi. Mila potofu bado zinaathiri haki za wanawake licha ya ukeketaji kudhibitiwa, mila hiyo haijakoma katika mikoa kama vile Arusha, Dodoma, Kigoma, Manyara, Mara na Morogoro, " alisema.

Balozi Mulamula alisema kongamano hilo ni njia nyingine ya kuonyesha kuwa mapambano dhidi ya unyanyasaji wa kijinsia yanaendelea na kuushukuru Ubalozi wa Ujerumani kwa kuhakikisha tukio hilo linafanyika kila mwaka.

"Wakati tunaadhimisha siku hizi (16 za ukatili) tukumbuke takwimu zinasemaje. Kati ya wanawake watatu, mmoja anapitia unyanyasaji wa kijinsia ikiwamo ukeketaji, na kupigwa," alisema Mulamula.

Aliongeza kuwa serikali inashirikiana na wadau wa kitaifa na kimataifa katika kupiga vita unyanyasaji wa kijinsia, ikiwa ni utekelezaji wa dira ya miaka mitano (2020-2025) inayohitaji kupambana na unyanyasaji wa kijinsia pamoja na mambo mengine.

Mkurugenzi Mkazi wa GIZ nchini, Dk. Mike Falke, alisema Ujerumani imetoa Sh. bilioni saba kuendeleza upatikanaji wa haki kwa wanawake na wasichana nchini.



"Msaada huu utasaidia kuboresha upatikanaji wa haki kwa wasichana na wanawake ili kuwakinga na unyanyasaji wa kijinsia kukuza usawa wa kijinsia nchini," alisema.

Naye Dk. Sheila Kawamara-Mishambi, Mkurugenzi Mtendaji wa Mpango wa Msaada wa Kanda ya Afrika Mashariki kwa Maendeleo ya Wanawake (EASSI), alisema uhamasishaji wa kutosha unatakiwa ili kubadilisha mtazamo wa watu kuhusu masuala ya unyanyasaji wa kijinsia.

Alisema vitendo vya unyayasaji haviripotiwi kwa sababu ya ukimya unaotokana na waathirika kuogopa jamii itawachukuliaje lakini pia hakuna adhabu zozote zinazotolewa dhidi ya wahusika.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**

**UCHAGUZI MDOGO WA UBUNGE JIMBO LA NGORONGORO NA UDIWANI KATA TANO (5)**

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inawatangazia wananchi wote wa Jimbo la Ngorongoro, Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro Mkoa wa Arusha pamoja na Kata tano (5) za Tanzania Bara kuwa kutakuwa na Uchaguzi Mdogo wa **Ubunge na Udiwani siku ya Jumamosi, tarehe 11/12/2021.** Kata zitakazofanya Uchaguzi ni Naumbu (Mtwara DC) Mtwara, Nyabulanda (Nyang'hwale DC) Geita, Likombe (Mtwara MC) Mtwara, Handali (Chamwino DC) Dodoma na Nalasi Mashariki (Tunduru DC) Ruvuma. Upigaji Kura utafanyika katika vituo vilivyotumika wakati wa Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020. Vituo vitafunguliwa saa moja kamili (1:00) Asubuhi na kufungwa saa kumi kamili (10:00) jioni. Utaratibu utakaofuatwa siku ya Uchaguzi ni kama ifuatavyo:-

1. **SIKU:** Wananchi watapiga Kura siku ya Jumamosi tarehe 11/12/2021
2. **VITUO:** Upigaji kura utafanyika katika vituo vilivyotumika wakati wa Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020
3. **MUDA:** Vituo vitafunguliwa saa 1:00 kamili Asubuhi na kufungwa saa 10:00 kamili Jioni

**Mambo ya kuzingatia wakati wa Uchaguzi.**

1. Mpiga Kura anatakiwa kutunza kadi yake ya kupigia kura aliyoitumia kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 na kuhakikisha anakwenda nayo kituoni siku ya uchaguzi.
2. Wapiga Kura waliopoteza kadi zao za kupigia kura au zilizoharibika, wanaruhusiwa kutumia mojawapo ya vitambulisho vifuatavyo:-
   - Hati ya kusafiria,
   - Leseni ya Udereva na,
   - Kitambulisho cha Uraia ambavyo majina yote matatu yafanane na yaliyomo kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura
3. Mpiga Kura anatakiwa kupanga mstari akiwa kituoni ambapo kutakuwa na mstari wa wanaume na wanawake.
4. Mpiga Kura awapo kituoni anatakiwa kutoa kipaumbele kwa Wapiga Kura wenye mahitaji maalumu kama vile Wazee, Wagonjwa, Watu Wenye Ulemavu, wajawazito na wenye watoto wachanga (watakaokuwa nao kituoni).
5. Ifikapo muda wa kufunga kituo saa 10:00 kamili Jioni kama Wapiga Kura bado wapo kwenye mstari, Mlinzi wa Kituo atasimama nyuma ya mtu wa mwisho na zoezi la upigaji kura litaendelea hadi wote wanamalizika. Mpiga Kura atakayefika zaidi ya muda wa kufunga kituo hataruhusiwa kupiga Kura.
6. Mpiga Kura anatakiwa afuate maelekezo yote atakayopewa na Msimamizi wa Kituo.
7. Baada ya kumaliza kupiga kura, Mpiga Kura anatakiwa kuondoka eneo la kituo cha kupigia kura.

Kumbuka kuzingatia kanuni za afya kwa kufuata maelekezo utakayopewa kituoni ili kujiepusha na maambukizi ya ugonjwa wa UVIKO-19 unaosababishwa na virusi vya virusi vya "corona"

**Gerald G. J. Mwanilwa**
**KAIMU MKURUGENZI WA UCHAGUZI**

Tangazo Hili Limetolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Eneo la uwekezaji Njedengwa, Kitalu D, Kiwanja Na. 4, Uchaguzi House, S. L. P 358, Dodoma. Barua Pepe:**uchaguzi@nec.go.tz**, **info@nec.go.tz**. **Tovuti: www.nec.go.tz**.

TANGAZO


NMB
Karibu yako
60
1961-2021
Benki ya NMB inawapongeza
Watanzania wote kuadhimisha
Miaka 60 ya Uhuru
COMPLETE
INDEPENDENCE
1961
www.nmbbank.co.tz

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Sherehe za mwisho wa mwaka zimekaribia, ila mahitaji ya shule kwanza*

**DESEMBA** huwa ni mwezi wenye shughuli nyingi zikiwamo sikukuu za mwisho wa mwaka ambazo huambatana na mahitaji ya fedha.

Shughuli hizo ni sikukuu ya Krismasi, kufunga mwaka na kuanza mwaka mpya pamoja na wazazi kuwajibika kupeleka watoto wao kuanza shule na wengine kuendelea na masomo.

Kwa maana hiyo Desemba I mwezi ambao watu kadhaa husafiri kutoka eneo moja kwenda lingine kwa ajili ya kuungana na jamaa, ndugu na marafiki kwa ajili ya kusherehekea Krismasi na shughuli za kuufunga mwaka na kufungua mwaka mwingine, hivyo fedha huhitajika kwa ajili ya usafiri na matumizi mengine.

Kwa upande mwingine, hata wasiosafiri huingia katika gharama za kununua mahitaji kama vyakula, mavazi na gharama nyingine. Uzoefu unatuonyesha kuwa kipindi hiki watu huhitaji fedha na hata wengine kukopa.

Mbali na fedha kwa ajili ya sikukuu, pia Desemba ni kipindi ambacho wazazi na walezi hukabiliwa na jukumu la kulipa ada za Januari kwa watoto wanaoanza chekechea, darasa la kwanza na kidato cha kwanza pamoja na wanafunzi wengine wanaorejea shule baada ya likizo. Watoto hawa sio tu wanahitaji kulipiwa karo pekee bali pia sare za shule na mahitaji mengine ya lazima pamoja na fedha binafsi kwa ajili ya matumizi kwa wanaoishi bweni.

Kwa watu ambao wana utaratibu wa kujiwekea akiba kwa ajili ya shughuli za Desemba na mwisho wa mwaka hawana tatizo, ila wasiokuwa na utaratibu wa kujiwekea akiba kidogokidogo hawa wana shida na kwa vyovyote wanakumbana na shida.

Kuanzia mapema wiki ijayo zitakuwa zimebakia wiki mbili kabla ya Krismasi, hivyo pilikapilika kuanza ikiwamo baadhi ya watu kusafiri kutoka eneo moja kwenda lingine kusherehekea.

Pamoja na umuhimu wa sherehe hizo, ni wajibu wa wazazi na walezi kukumbuka kwamba suala la shule ni muhimu, kwa maana ya gharama zinazohitajika kuwa zimekamilishwa kabla ya mambo mengine.

Elimu ndio uwekezaji na urithi kwa mtoto wake au mtoto anayemlea, hivyo maandalizi ya shule kwa mwakani yanapaswa kukamilishwa mapema ili kujiepusha na usumbufu wa mtoto kukataliwa kupokelewa shuleni kwa sababu za kutokukamilisha mahitaji muhimu.

Gharama za shule haziwezi kuepukwa kwa sababu hakuna mmiliki wa shule ambaye atakubali kumpokea mtoto ambaye hajalipa karo na mahitaji mengine muhimu kwa kuwa shule zinaendeshwa kwa gharama kubwa.

Kutokana na hali hiyo, tunawashauri wazazi na walezi waanze sasa kufanya mandalizi ya kujiwekea akiba kidogo ili Januari ikifika wawe wamekamilisha mahitaji hayo na watoto wao wapokelewe na kuanza masomo bila mkwamo wowote.

Hatusemi kwamba watu wasisherehekee, bali tunashauri wafanye hivyo, lakini kipaumbele kiwe elimu kwa watoto wao, tukiamini kuwa sherehe ni mambo ya kupita tu ila elimu ni suala muhimu na endelevu.

Baadhi ya mataifa jirani zetu yanalitambua hilo, hivyo kuamua kulipa suala la elimu kipaumbele, ikiwamo kuwekeza na kupeana sapoti kupitia michango ya harambee ili kusomesha watoto ikiwamo kuwapeleka ng'ambo.

Ni wakati mwafaka sasa na sisi kama taifa kuona umuhimu wa elimu kabla ya mambo mengine, kwa kutambua kuwa ndio ufunguo wa maisha kupitia kuwekeza katika sekta hiyo kwa urithi wa watoto wetu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# *Miaka 60 ya Uhuru imevuka salama, kilichoko 'kazi iendelee' mbele zaidi*

Na Jenifer Gilla

**DESEMBA** 9, mwaka 1961, Tanganyika ilishusha chini bendera ya mkoloni na kuipandisha ya taifa huru pamoja na Mwenge wa Uhuru, kwenye kilele cha Mlima Kilimanjaro, ikiwa ni ishara kuwa na taifa huru lenye kufanya mambo yao wenyewe.

Jana, Tanganyika ilitimiza miaka 60 ya Uhuru ikiwa ndani ya jina jipya la Tanzania baada ya kuungana na Zanzibar miaka 57 iliyopita. Hapo kuna mafanikio lukuki yaliyotokana na juhudi zake yenyewe, chini ya viongozi bora waliochaguliwa na wananchi kwa Uhuru.

Iwapo hujui, dodosa maudhui ya Muungano, faida zilizofikiwa na kero zinazojitokeza na kufanyiwa kazi kwa ustadi mkubwa, kuhakikisha zinapunguzwa kuelekea kumalizwa.

Katika hotuba yake juzi usiku, Rais Samia Suluhu Hassan alisema Watanzania wana kila sababu ya kutembea kifua mbele, kutokana na mafanikio makubwa iliyoyapata ndani ya kipindi hicho.

Aliyataja baadhi kuwa ni kulinda uhuru wa nchi na mipaka yake, kujenga umoja wa kitaifa, amani, utulivu na mshikamano wa wananchi, kuimarisha uchumi na kupunguza umaskini.

Rais alitaja mafanikio mengine kuwa ni kuongeza upatikanaji na kuboresha huduma kwa wananchi, kujenga heshima ya nchi, ushawishi kikanda na kimataifa na kuimarisha demokrasia na utawala wa sheria nchini.

Pia alisema uchumi wa nchi umekua, hata leo hii nchi inajinasibu imeingia kwenye uchumi wa kati kabla ya mwaka uliokusudiwa (2025), huku mwaka1961 uhuru ulipopatikana, wastani wa pato la mwananchi likikuwa kutoka Sh.776 kwa mwaka, hadi Sh. milioni mbili mwaka jana, 2020.

Rais pia alijivunia maboresho ya huduma za kijamii ikiwamo elimu, akitoa mfano sasa kuna vyuo vikuu 30, kati yake 18 vikimilikiwa na serikali, mamilioni ya wanafunzi kwenda sekondari, hospitali za kibingwa zipo tano na hospitali ya taifa moja, kuimarishwa huduma ya maji na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Hakika ni jambo la kujivunia, kwa kuwa bado kuna nchi zinapambana kufikia hatua ambayo Tanzania ipo kwa sasa. Lakini, ni muhimu kukumbushana kwamba, si kigezo cha kuzembea kwa kudhani kuwa kazi imekwisha, bado tuna kazi kubwa ya kufanya kuhakikisha tunasongambele zaidi, hata kufikia uchumi wa juu.

Bado kuna mambo yanaonekana kikwazo katika kufikia uchumi wa juu, ikiwamo baadhi ya shughuli za kijamii kuwa duni.

Katika hotuba yake, Rais Samia alisema kuwa hali ya udumavu nchini bado si nzuri, akiitaka Taasisi ya Chakula na Lishe (TFNC) kuchukua hatua za kukabiliana na adha hiyo.

Kwa mujibu wa takwimu za lishe ya mwaka 2019/2020, mikoa inayozalisha chakula kwa wingi, ndiyo yenye viwango vikubwa vya udumavu kwa watoto, mfano hai Njombe ina udumavu wa asilimia 53.6, wakati uzalishaji wa mazao tani 446,491 kuwa na kiwango cha utoshelevu- (SSR) asilimia 194 na Mkoa wa Rukwa asilimia 47.9, huku uzalishaji ni tani 943,002 na kiwango cha utoshelevu asilimia 230.

Kila mmoja kwa nafasi yake nchini, anapaswa kuwajibika na kuhakikisha tunamaliza changamoto hiyo, pamoja na nyinginezo kama athari za mabadiliko ya tabianchi, ambayo unaitesa dunia kwa sasa, inayoweza kuchangia ongezeko la udumavu kama isipodhibitiwa vilivyo.

Tuungane kwa vitendo na kauli ya Rais Samia Suluhu ya 'Kazi Iendelee', ikiwa na maana ya kuendelea pale tulipoishia kwa kasi ileile au zaidi, ili kufika pale taifa linapokusudia na kwa rehema zake Mwenyezi Mungu mwakani, tutakapoadhimisha sherehe hizi tufurahie mafanikio zaidi.

# TANGAZO

Bagamoyo Sugar Limited
Bagamoyo, Tanzania, East Africa

**"WANTED FOR SUGAR PLANT & COGENERATION PLANT"**

**JOB VACANCIES**

We are establishing a new green field project of 1500 tcd expandable to 2500 tcd Sugar plant with 5 MW Cogeneration at Makurunge District – Bagamoyo, Tanzania.
Applications are invited for the following positions:

## SUGAR & COGENERATION PLANT

### SUGAR PLANT : MANUFACTURING / PROCESS

| S/No | NAME OF THE POST | QUALIFICATION | EXPERIENCE | REQUIRED POSTS |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Shift MFG Chemist (Sugar) | B.Sc. (Sugar Tech) | 8 - 10 Years | 2 |
| 2 | Lab Chemist (WTP & ETP) | B.Sc. | 5 - 8 Years | 2 |
| 3 | Juice Supervisor | Diploma/Above | 8 - 10 Years | 2 |
| 4 | Evaporate Mate | Diploma/Above | 8 - 10 Years | 2 |
| 5 | Vacuum Filter Mate | Diploma/Above | 8 - 10 Years | 2 |
| 6 | SRTC (Juice Clarifier) Mate | Diploma/Above | 8 - 10 Years | 2 |
| 7 | MOL Station Operator | Diploma/Above | 5 – 6 Years | 2 |
| 8 | Pan In charge | Diploma/Above | 8 - 10 Years | 1 |
| 9 | Pan man | Diploma/Above | 8 - 10 Years | 4 |
| 10 | Batch machine Operator / C/F Operator- "A" | Diploma/Above | 5 - 6 Years | 2 |
| 11 | Continuous Machine Operator | Diploma/Above | 5 - 6 Years | 4 |
| 12 | Crystallizer Attendant | Diploma/Above | 5 - 6 Years | 3 |
| 13 | Magma Attendant | Diploma/Above | 5 - 6 Years | 3 |
| 14 | Melter Attendant | Diploma/Above | 5 - 6 Years | 3 |
| 15 | Hopper Attendant | Diploma/Above | 5 - 6 Years | 3 |
| 16 | Sugar House Clerk | B. Com | 5 - 6 Years | 1 |
| 17 | Sugar House Helper | Diploma/Above | 2 – 3 Years | 4 |
| 18 | Lab Boy Technician | Diploma/Above | 2 - 3 Years | 3 |
| 19 | Centrifugal Helper | Diploma/Above | 2 – 3 Years | 4 |
| 20 | Pan Helper | Diploma/Above | 2 - 3 Years | 4 |
| 21 | WTP Operator | Diploma – Science or BSc | 4 - 5 Years | 3 |
| 22 | ETP Operator | Diploma – Science or BSc | 4 - 5 Years | 3 |
| 23 | WTP/ETP Helper | Diploma/Above | 2 - 3 Years | 6 |

### SUGAR PLANT : ENGINEERING – MILL HOUSE

| S/No | NAME OF THE POST | QUALIFICATION | EXPERIENCE | REQUIRED POSTS |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Shift Engineer (Mill) | BA Mech / DME | 8 - 10 Years | 1 |
| 2 | Shift Engineer (Process House) | BA Mech / DME | 8 – 10 Years | 1 |
| 3 | DCS Operator Mill house | BA Mech / DME | 6 - 8 Years | 2 |
| 4 | Draftsman Mechanical | Diploma / Certificate | 6 – 8 Years | 1 |
| 5 | Mill Fitter A Grade | Certificate - Fitter | 8-10 Years | 1 |
| 6 | Mill Fitter B Grade | Certificate- Fitter | 4-5 Years | 1 |
| 7 | Hilo Unloader Operator | Certificate- Fitter | 4-5 Years | 2 |
| 8 | Feeder Table Operator | Certificate- Fitter | 4-5 Years | 3 |
| 9 | Mill Oilman | Certificate- Fitter | 4-5 Years | 2 |
| 10 | Welder | Certificate in Welding or Equivalent | 4-5 Years | 3 |
| 11 | Mill Fitter Helper | Certificate- Fitter | 4-5 Years | 6 |
| 12 | Boiling House Fitter | Certificate Fitter | 5 - 6 Years | 2 |
| 13 | Centrifugal Fitter | Certificate Fitter | 5 - 6 Years | 2 |
| 14 | Workshop Machinist | Certificate Turner | 5 - 6 Years | 1 |
| 15 | Workshop Turner | Certificate Fitter | 5 -6 Years | 2 |
| 16 | Fitter B Grade (Boiling House) | Certificate Fitter | 3 - 4 Years | 3 |
| 17 | Workshop Helper | Certificate Fitter | 2 - 3 Years | 4 |
| 18 | Fitter Helper | Certificate Fitter | 2 - 3 Years | 8 |
| 19 | Store Keeper | Graduate Bachelor Degree | 6 – 8 Years | 1 |
| 20 | Store Assistant | Diploma/Above | 3 -4 Years | 2 |
| 21 | Store Assistant Helpers | Diploma/Above | 1 -2 Years | 2 |

### SUGAR PLANT : ELECTRICAL & INSTRUMENTATION

| S/No | NAME OF THE POST | QUALIFICATION | EXPERIENCE | REQUIRED POSTS |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Instrument Junior Engineer | Diploma - BA Instrumentation | 6-8 Years | 1 |
| 2 | Electrical Jr. Engineer | Diploma / BA - Electrical | 5 -6 Years | 1 |
| 3 | Instrument Technician / Mechanic | Certificate– Instrumentation /Electrical | 6-8 Years | 2 |
| 5 | Weigh Bridge operator | Certificate– Instrumentation /Electrical | 2 – 3 Years | 2 |
| 6 | Electrician | Certificate Electrical | 8-10 Years | 2 |
| 7 | Wireman | Certificate Electrical | 5-6 Years | 3 |
| 8 | Switch Board Operator | Certificate Electrical | 5-6 Years | 3 |
| 9 | Line Supervisor | Certificate Electrical | 6 -8 Years | 1 |
| 10 | Lineman | Certificate Electrical | 5-6 Years | 1 |
| 11 | Wireman Helper | Certificate Electrical | 2-3 Years | 6 |
| 12 | Instrument Technician Helper | Certificate– Instrumentation /Electrical | 2-3 Years | 3 |
| 13 | AC Technician | Certificate- Instrumentation /Electrical | 4 -5 Years | 1 |
| 14 | AC Technician Helper | Certificate - Instrumentation /Electrical | 1 -2 Years | 1 |

### SUGAR PLANT : ENGINEERING

| S/No | NAME OF THE POST | QUALIFICATION | EXPERIENCE | REQUIRED POSTS |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Shift Engineer (Boiler & Turbine) | BA Mech / DME | 8 - 10 Years | 2 |
| 2 | DCS Operator (Boiler) | BA Mech / DME | 8 - 10 Years | 2 |
| 3 | DCS Operator (Turbine) | BA Mech / DME | 8 - 10 Years | 2 |
| 4 | Boiler Attender or Operator | Certificate Fitter or Equivalent | 8 - 10 Years | 2 |
| 5 | Turbine Attender or Operator | Certificate Fitter or Equivalent | 8 - 10 Years | 2 |
| 6 | Turbine Oilman | Certificate Fitter or Equivalent | 5 - 6 Years | 2 |
| 7 | Boiler Fitter A Grade | Certificate Fitter or Equivalent | 5 - 6 Years | 2 |
| 8 | Boiler fitter B Grade | Certificate Fitter or Equivalent | 5 - 6 Years | 3 |
| 9 | Boiler Fireman | Certificate Fitter or Equivalent | 5 - 6 Years | 4 |
| 10 | Feed Water Pump Attendant | Certificate Fitter or Equivalent | 5 - 6 Years | 3 |
| 11 | Bagasse Yard Supervisor | Certificate Fitter or Equivalent | 5 - 6 Years | 3 |
| 12 | Bagasse handling Operator | Certificate Fitter or Equivalent | 5 - 6 Years | 3 |
| 13 | Ash handling Operator | Certificate Fitter or Equivalent | 5 - 6 Years | 3 |
| 14 | Welder IBR / General (Each one) | Certificate Fitter or Equivalent | 5 - 6 Years | 2 |

Interested and eligible candidates may send their Resume/CV by Email along with Testimonials, Salary Proof, Qualification & Experience Certificates on Email ID **recruitment@bagamoyosugar.com** on or before **30 .12.21.** Only Candidates that meet above criteria will be called for interview.

The management has the right to accept or reject all or any application without assigning any reason.

***HR Manager Bagamoyo Sugar Ltd***

@bagamoyosugarlimited



# Sekta ya Utalii haijatangazwa ipasavyo kwa miaka 60

**Na Christina Mwakangale**

SERIKALI imesema pamoja na nchi kufikisha miaka 60 ya uhuru na kuwa moja ya nchi zenye vivutio vingi vya utalii, duniani, bado havijatangazwa ipasavyo na kulipa taifa tija kiuchumi.

Katibu Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk Allan Kijazi, aliyasema hayo juzi, jijini Dar es Salaam, kwenye kongamano la kuadhimisha miaka 60 ya Uhuru wa Tanganyika na kuzingatia ukuaji katika sekta ya utalii na ukarimu, fursa na changamoto kwa kipindi hicho, lililoandaliwa na Chuo cha Taifa cha Utalii (NCT).

Alisema pamoja na miaka 60 ya uhuru, nchi inahitaji kufanya zaidi ili kuongeza pato la taifa.

Dk. Kijazi alibainisha kuwa ili nchi kuongeza pato, kuna haja ya serikali kushirikiana na sekta binafsi kuvitangaza vivutio na kuendeleza utalii na kwamba wahitimu wa elimu ya juu, wawe wabunifu na kutoa mchango wa ukuaji sekta hiyo.

"Tunahitaji kuimarisha utangazaji wa vivutio vya utalii ndani na nje ya nchi. Serikali imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwamo kuandaa na kushiriki kwenye makongamano, maonyesho na ziara za utangazaji utalii katika masoko msingi na kimkakati.

"Tunaimarisha matumizi ya (teknolojia ya habari na mawasiliano) TEHAMA, kuandaa ziara za mafunzo kwa waandishi wa habari wa kimataifa, mawakala wa utalii na usafirishaji kwa ajili ya kusaidia kutangaza utalii wa nchi," alisema Dk. Kijazi.

Pia alisema kwamba Watanzania wajenge utamaduni wa kufanya utalii wa ndani, akisema asilimia mbili kati ya Watanzania milioni 60, wakitembelea maeneo yenye vivutio, itaifikia idadi ya watalii ambao walifika nchini mwaka 2019 waliokuwa milioni 1.5.

Ofisa Mtendaji Mkuu NCT, Dk Shogo Mlozi, alisema lengo la kongamano hilo ni kuongeza fursa pamoja na kukabiliana na changamoto zilizopo kwenye sekta ya utalii.

"Chuo kimepiga hatua kimkakati na kuongeza kampasi hadi nne nchini, program zimeongezwa zipo 18 ikiwamo ya uanagenzi.

Ajira kwenye sekta ni milioni 1.6, kati yao, laki sita wameajiriwa moja kwa moja katika sekta na ambao wameajiriwa na sekta inayohusiana na sekta hiyo ni milioni moja," alisema Dk Mlozi.


NIC Life House 4th Floor, Wing C
Sokoine Drive/Ohio Street,P. O. Box 6100,Dar es Salaam
Tel:+255 22 2112045,Fax: +255 22 2112045

Dev Recoveries Ltd

**NOTISI YA KULIPA DENI NA MNADA WA HADHARA**

Kampuni ya **DEV RECOVERIES LIMITED** kwa idhini tuliyopewa na **EQUITY BANK TANZANIA LIMITED,** tunatoa notisi ya siku kumi na nne ya kulipa deni kwa hiari muda huo ukifika bila kulipa dhamana itauzwa kwa njia ya **MNADA WA HADHARA,** Mnada utafanyika siku na tarehe kama inavyoonekana hapo chini, mnada utafanyika kuanzia saa 6:00 mchana na kuendelea mahali dhamana ilipo kama inavyoonyesha hapo chini.

**MCHANGANUO WA DHAMANA ITAKAYOUZWA .**

| NA | JINA LA MDAIWA | DHAMANA/MAHALI ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| 1. | OCEANIC RESORT/ FLORENCE RWENYEMAMU FRANCIS | Hati Na. 79320, Kiwanja No.1042-49, Kitalu "B" Mbweni, Dar es Salaam City. Ukubwa wa eneo sqm 10,500. | 29/12/2021 kuanzia saa 06:00 mchana |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Dhamana itauzwa "kama ilivyo".
2. Mnunuzi atatakiwa kulipia 25% ya bei ya mnada siku ya mnada na kiasi cha pesa kilichobaki kilipwe ndani ya siku 14, kinyume cha hapo kiasi kilichotolewa awali hakitarudishwa na mnada utarudiwa tena
3. Gharama za kubadilisha hati miliki (transfer of ownership) na gharama nyingine ni za mnunuzi.
4. Ukaguzi wa dhamana utafanyika kuanzia siku ya tangazo hili kutoka kuanzia saa 02:00 asubuhi na kuendelea.
5. Kwa mawasiliano zaidi piga **simu No: 0788438640 / 0712390460**




Ofisa Huduma kwa Wateja wa Benki ya NMB Makao Makuu, Neema Kazoviyo (kushoto), akizungumza na mshindi wa droo ya kampeni ya Bonge la Mpango kwa njia ya simu baada ya kuibuka mshindi katika droo hiyo, jijini Dar es Salaam juzi. Katikati ni Meneja wa NMB Tawi la Bank House, Seka Urio na Msimamizi kutoka Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania, Elibariki Sengasanga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wadau wafunguka upangaji machinga

**Na Anaeli Mbise**

BAADA ya Rais Samia Suluhu Hassan, kuwatoa hofu machinga kuwa hawatajutia uamuzi wa serikali wa kuwahamishia maeneo maalumu, huku akiahidi kuwa mambo mazuri yanafuata kwao, baadhi ya wafanyabiashara hao na wadau wamefunguka.

Wameshauri kuhusu namna ambavyo serikali inatakiwa kuweka mazingira yaliyo rafiki ya ufanyaji wa biashara hizo.

Akizungumza na Nipashe jana, Sabatho Nyamsenda, kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), alitoa ushauri wa namna ambavyo wataalamu wa mipango miji na halmshauri wanavyotakiwa kuweka mazingira wezeshi kwa wamachinga kufanya biashara ikiwamo kutengeneza maeneo bora na ambayo ni mali ya wote.

"Ukweli ni kwamba katika kuwaondoa wamachinga kuna namna ambavyo mabavu yametumika na hata wengine kupoteza bidhaa zao. Hili suala la kuwapanga katika maeneo maalumu halikuzingatia uhalisia wa biashara ya umachinga ambayo ni kupanga bidhaa katika maeneo yenye mzunguko mkubwa wa watu ili kupata wateja," alisema Nyamsenda.

Alisema pia ni wakati sasa wa kubadili mtazamo juu ya upangaji wa miji ili kutumia dhana ya haki-jiji kwa wote kwa kuzingatia demokrasia shirikishi na matamanio ya watu wa tabaka la chini juu ya namna ambavyo miji inapaswa kuwa.

"Serikali pia inatakiwa kuangalia namna ya kutenga maeneo kwa ajili ya wenye ulemavu ambalo ni kundi linalosahaulika ikiwamo pia kuheshimu usawa wa kijinsia kwa wote pasipo kuwa na ubaguzi wa aina yeyote," alisema.

"Halmashauri zitakapokuwa zinafanya ujenzi wa miundombinu kama barabara na vituo vya daladala zinatakiwa kuacha maeneo ya wazi angalau mita mbili hadi tatu kutoka kila upande wa barabara kwa ajili ya sehemu za wafanyabiashara wadogo kufanya kazi zao za kujipatia kipato," aliongeza Nyamsenda.

Dk. Abunuwasi Mwami, kutoka Chuo Kikuu Kishiriki cha Jordan Morogoro, alipendekeza ni vyema serikali ikalinda tabaka hilo la wafanyabiashara wadogo ambao ndiyo wavuja jasho kwa kuwatengea maeneo hayo kwa sababu wanategemea kupata kipato cha kuishi kama binadamu wengine kutokana na biashara hizo.

Alisema pia ni vyema serikali ikaangalia namna ya kuondoa matabaka katika jamii kati ya wanaoishi uzunguni, uhindini pamoja na uswahilini wote wapewe fursa na mamlaka za miji na halmashauri kufanya biashara kwa usawa.

"Biashara lazima ifuate watu japo kuwa miji yetu mingi imekaa kikoloni na siyo miji ya uzalishaji kama ilivyokuwa Manchester zamani ...hii ni lazima mamlaka ziangalie namna ya kuwawezesha hawa machinga nao wafaidi matunda ya kutumia ardhi yao," alisema Dk. Mwami.

Mwenyekiti wa wafanyabiashara wadogo katika eneo la Kivukoni Mkoani Dar es Salaam, Catherine Bundala, alisema jambo la kuwapanga machinga ni kitu kizuri, lakini tatizo kubwa ni namna ambavyo wanaotekeleza jukumu hilo wanatakiwa kuangalia namna bora ya upangaji wa biashara hizo.

"Kama mimi nauza nyanya unanipeleka Machinga Complex ghorofa ya tano wakati chini wapo wanaouza hiyo hiyo bidhaa ya nyanya hii haijakaa sawa. Kwahiyo ungetumika utaratibu wa aina ya biashara kuwa sehemu moja hata kama tungekuwa ghorofa ya tano wateja watakuja sababu chini hiyo bidhaa hamna," alisema Bundala.

Naye, Mwenyekiti wa machinga katika eneo la Gongo la Mboto wilayani Ilala jijini Dar es Salaam, Christoher Kidiga, alisema maeneo ya kupangiwa wafanyabiashara hao hayajapatikana, lakini baadhi ya watendaji wa serikali wameanza kukamata bidhaa zao pasipo kufuata utaratibu.

# Elimu ujasiriamali kupunguza umaskini

**Na Elizabeth Zaya**

OFISA Maendeleo ya Jamii Manispaa ya Mpanda, Marietha Mkozi, amesema elimu ya ujasiriamali kwa vijana na wanawake ni muhimu kwa kuwa itasaidia kupunguza umaskini na kuwaondoa katika hatari ya kuingia kwenye vishawishi vya uhusiano wa kimapenzi.

Aliyasema hayo jana mkoani Katavi katika semina ya kuwajengea uwezo vijana na wanawake namna ya kuendesha biashara ndogo kwa kuomba mikopo kwenye taasisi za fedha na taasisi za umma, usafi wa mzingira, afya ya uzazi na ujinsia pamoja na namna ya kujikinga na ugonjwa wa COVID-9 iliyodhaminiwa na taasisi ya inayojishughulisha na kuwajengea uelewa vijana juu ya uzazi salama (HCCGWT).

Mkozi alisema vijana wanapojishughulisha na kazi mbalimbali ikiwamo kuingia kwenye biashara hususani wa kike, wanakuwa na uwezekano mkubwa wa kukwepa vishawishi ambavyo vimekuwa vikiwasababishia baadhi yao kuambukizwa maradhi ikiwamo virusi vya Ukimwi.

Pia alisema wanapojiunga katika vikundi mbalimbali vya biashara, wanajifunza mambo mengi ya kibiashara na namna ya kutafuta masoko na kuboresha zaidi biashara zao.


"Na kwenye mafunzo kama haya tunawafundisha vijana hawa namna ya kuwa na malengo na kuendesha biashara ambazo ni mahitaji ya kila siku kwenye jamii, kuhakikisha wanakuwa wabunifu, kubuni mawazo mapya kila siku na kutoa huduma bora na kuziongezea thamani bidhaa zao," alisema Mkozi.

"Tunawaelimisha kwamba wazo lolote la biashara halitaleta matunda chanya endapo halitafanywa kwa ubunifu na umakini zaidi," aliongeza.

Mkurugenzi Mtendaji wa HCCGWT, Halima Lila, alisema vijana na wanawake 40 walipewa mafunzo hayo kutoka katika mkoa huo wa Katavi.

Alisema kupitia mafunzo hayo, vijana wengi walisema wako tayari kuwa mabalozi wa kutoa elimu kwa wenzao kuhusu namna ya kuanzisha biashara ndogo wakiamini ndilo suluhisho la kupunguza mimba za utotoni zinazosababishwa na vijana wengi kujiingiza katika mahusiano ya kimapenzi mapema.

"Na kupitia mafunzo haya, tayari baadhi yao wameanza kujiunga katika vikundi vya ujasiriamali kwa ajili ya kuanzisha biashara zao na tunaamini kupitia vikundi hivyo watapata uzoefu, watakuwa wazalishaji wakubwa na wataondokana na umaskini," alisema Lila.




Mkurugenzi wa Airtel Money Tanzania, Isack Nchunda (kulia), akigongeshana mkono na Mwenyekiti wa Bodi wa Benki ya Letshego, Simon Njengo (katikati), katika uzinduzi wa huduma ya "Kuza Akiba Ushinde", jijini Dar es Salaam juzi. Kushoto ni Mkurugenzi Mkuu wa benki hiyo, Omar Msangi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# NMB Bonge la Mpango yatoa zawadi za mil. 23/- kwa mpigo

**Na Mwandishi Wetu**

ILE kampeni ya Weka Akiba na Ushinde inayoendeshwa na Benki ya NMB 'NMB Bonge la Mpango,' imezidi kushika kasi, baada ya wiki hii kumwaga zawadi zenye thamani ya Sh. mil. 23.5 kwa mpigo, hivyo kufanya thamani ya jumla ya zawadi zote kufikia Sh. milioni 117 katika kipindi cha wiki 9.

Droo mbili kwa mpigo za 'NMB Bonge la Mpango - 2merudi Tena,' zimefanyika Jumatano jijini Dar es Salaam, ikiwamo ya mwisho wa mwezi (Novemba) iliyotoa zawadi za pikipiki tatu za mizigo aina ya Skymark na droo ya wiki ya 9 iliyotoa washindi 12, kati ya hao 10 wakishinda pesa taslimu na wawili wakijinyakulia pikipiki hizo miguu mitatu.

Katika droo hiyo iliyofanyika chini ya usimamizi wa Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania (GBT), Saleh Omari (wa Tawi la Chakechake), Kelvin Masava (Mwenge) na George Nyaisonga (Mbalizi Road), walitangazwa washindi wa mwisho wa mwezi Novemba wa pikipiki za mizigo zenye thamani ya Sh. milioni 4.5 kila moja.

Nao Ludovick Damas (Masasi) na Ally Mnyone (Tawi la Madaraka), waliibuka washindi wa pikipiki mbili za droo ya tisa, iliyotoa pia washindi 10 wa pesa taslimu, wakiwamo Luqman Khamis (Congo Street), Wilfred Rajabu (Mlimani City) na Alberth Fanuely (Madaraka).

Washindi wengine wa pesa taslimu waliopatikana katika droo ya tisa ni pamoja na Ramadhani Maambe (Chalinze), Upendo Israel (Kahama), Rashid Mussa (Lindi), Melkiory Mholya (Songea), Victoria Bunyinyiga (Tarime), Msafiri Daffa (Wami) na Meshack Jonathan (SM-Kenyatta Road).

Aidha, pikipiki tano za mizigo zilizotolewa wiki hii, zinafanya kampeni hiyo hadi sasa kuwa imeshatoa jumla ya pikipiki 24 zenye thamani ya Sh. milioni 108 kati ya pikipiki 50 zitakazotolewa katika kampeni yote, ambako zawadi za pesa taslimu zimefikia Sh. milioni 9, hivyo thamani ya jumla ya zawadi zote kufikia Sh. milioni 117.

Kwa sasa NMB Bonge la Mpango imebakisha pikipiki 26 zenye thamani ya Sh. 117 zinazoshindaniwa, sambamba na pesa taslimu Sh. milioni tatu zitakazoenda kwa washindi 30 wa wiki tatu zilizobaki kuhitimisha kampeni hiyo ambayo ina zawadi zenye thamani ya Sh. milioni 237.

## Airtel, Letshego zaja na kampeni ya akiba

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya simu za mkononi ya Airtel Tanzania leo imetangaza kuzindua kampeni ya kuweka akiba – "Kuza Akiba Ushinde na Timiza Akiba" ambapo wateja wa Airtel Money watapata fursa ya kushinda hadi 20,000 kila wiki pale wanapoweka akiba kwenye akaunti ya Timiza Akiba na bila kutoa kwa wiki hiyo.

Timiza Akiba ambayo ni akiba ambayo inapatikana kwa simu za mkononi kwa wateja wote wa Airtel Money, ni rahisi kutumia na inatoa riba kwa kila mwezi kwa kila anayewekeza, ambayo hutolewa kulingana na kiasi kilichoko kwenye akaunti ya Timiza Akiba na hutolewa kwa lengo la kuhamasisha Watanzania kujenga utamanduni wa kujiwekea akiba.

Akizungumza leo jijini Dar es Salaam wakati wa kutangaza kuzindua kampeni hiyo, Mkurugenzi wa Airtel Money Isaack Nchunda, alisema: 'Kampeni hii ina lengo la kuhamasisha utamanduni wa kuweka akiba kwa wateja wa Timiza Akiba na vile vile kuwavutia wateja wengine wapya. Tunaendelea kutoa wito kwa Watanzania kuendelea kujenga utamanduni wa kuweka akiba alisema Nchunda huku akiongeza kuwa Airtel Tanzania imeshirikiana na Letshego Bank kuendesha kampeni hii."

Nchunda aliongeza kuwa letu ni kuwahimiza wateja wetu waendelee kuweka akiba zaidi kwenye akaunti zao za Timiza Akiba kupitia Airtel Money na kwa wateja wapya kufungua akaunti na kuanza kuweka akiba kwenye Timiza Akiba ili kupata nafasi ya kushinda hadi Sh. 20,000 kila wiki.

Akizungumzia jinsi washindi watakapokuwa wanapatikana, Nchunda alisema kuwa mteja yeyote wa Airtel Money anayeweka Sh. 20,000 kwa wiki kwenye akaunti ya Timiza Akiba atakuwa na nafasi ya kuingia kwenye droo na kushinda mara moja kwa wiki. Aliongeza, 'Washindi 25 watakuwa wakipatakana kila wiki kupitia droo itakayokuwa ikiendeshwa na Airtel katika wiki sita za kampeni hii. Washindi hao watapata zawadi zao za Sh. 20,000 kila mmoja kupitia akaunti zao za Airtel Money.

Mkurugenzi Mtendaji wa Letshego Benki Tanzania, Omar Msangi, alisema wameamua kushirikiana na Airtel kuendesha kampeni hiyo ili kuungana mkono jitihada za kuleta suluhisho la huduma za kifedha nchini pamoja na kuendelea kujenga utamanduni wa kuweka akiba kwa Watanzania.

"Tunatoa rai kwa Watanzania kuendelea kujenga utamanduni wa kujiwekea akiba kwa matumizi ya baadaye. Pia naomba niwaakikishie kuwa washindi wote watapata zao kupitia akaunti zao za Airtel Mone," alisema na kuongeza:

"Timiza Akiba ni matokeo ya chanya ya kushirikiana na Airtel ambayo inaonyesha jinsi Letshego ilivyojipanga kuinua maisha. Ushirikiano huu kwetu unabaki kuwa ni nyenzo muhimu sana kwetu pamoja na Airtel, tutaendelea kuwaamasisha Watanzania waendelee kuwejenga utamanduni wa kujiwekea akiba kidigitali popote pale."

# DC ahimiza tahadhari corona

**Thobias Mwanakatwe**

MKUU wa Wilaya ya Iringa, Mohamed Moyo, amewataka wananchi kuendelea kuchukua tahadhari zinazotolewa na wataalamu wa afya kutokana na kuibuka kwa wimbi la nne la ugonjwa wa corona.

Alisema hayo juzi wakati akizungumza na wananchi kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika kata za Mshindo na Miyomboni - Kitanzini ambao pia uliohudhuriwa na Meya wa Manispaa ya Iringa, Ibrahim Ngwada, kwa lengo la kusikiliza kero za wananchi na kuzipatia ufumbuzi.

Moyo alisema wakati wakiendelea kuchukua tahadhari ya wimbi hilo ambalo lilianza kujitokeza mwishoni mwa Oktoba, mwaka huu, wananchi wanapaswa kuendelea kujitokeza kupata chanjo ambazo zinatolewa bure kwenye vituo vya afya wilayani humo.

Aidha, aliwapongeza madiwani kwa jinsi wanavyoendelea kusimamia miradi ya ujenzi wa shule za misingi, sekondari na vituo vya afya inayojengwa chini ya fedha za UVIKO-19 zilizotolewa na serikali kuu.

Kuhusu sensa ya watu na makazi inayotarajia kufanyika mwakani, Moyo aliwataka wananchi kuwapa ushirikiano makarani wa serikali ili kupata takwimu na ifikapo muda huo watu wote wanapaswa kuwa katika makazi yao husika.

Meya Ngwada alimweleza mkuu huyo wa wilaya kuwa manispaa hiyo inatekeleza miradi ya UVIKO-19 kwa kujenga madarasa 33 na kituo cha afya cha kisasa, zahanati ya Mkimbizi na ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami katika Kata ya Mtwivila.

Ngwada alisema Manispaa pia imepokea pesa kutoka serikali kuu kwa ajili ya kuboresha ujenzi wa jengo la Community Centre.

Aliongeza kuwa halmashauri pia itahakikisha miradi yote inayojengwa kwa fedha za ndani kama vile ujenzi wa soko la Mlandege na stendi ya Igumbilo inakamilika kwa wakati.

Nao wananchi waliwasilisha kero zao kwa viongozi hao, huku Augustino Sambagi alielezea kero ya maji kwa wasomaji wa mita kuongeza idadi ya namba za mita na kuleta changamoto kwa kuwa gharama zinazokuja ni kubwa kulinganisha na matumizi ya maji wanayotumia wananchi.

Sambagi pia alizungumzia suala la kupanda kwa bei ya pembejeo kama mbolea hali ambayo imesababisha kilimo msimu huu kuwa kigumu.

Naye Shabani Borakupata, alisema miundombinu bado ni tatizo kwa kuwa barabara zimekuwa mbovu na kuwa kero kwa wananchi na kuiomba serikali kuangalia uwezekano wa kuzijenga kwa kiwango cha lami.

Akijibu kero hizo, Moyo alisema serikali imezichukua na kuwaahidi kuwa itazifanyia kazi.




Mkurugenzi wa Biashara na Uwekezaji wa Shirika la Bima Zanzibar, Mohammedi Ameir (wapili kushoto) pamoja na maofisa wenzake, wakionyesha kwa waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, mipira maalumu iliyohifadhi namba tofauti za kiasi cha mafuta kitakachotolewa kwa washindi wa kampeni ya "Wese Ndio Mchongo", inayotoa fursa kwa wateja wa shirika hilo kote nchini kujaziwa mafuta kwenye vyombo vyao vya usafiri ikiwa ni zawadi kwao katika kuadhimisha ya miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara pamoja na miaka 58 ya Mapinduzi ya Zanzibar. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wateja wa bima kuzawadiwa mafuta

**Na Elizabeth Zaya**

SHIRIKA la Bima la Zanzibar (ZIC) limezindua kampeni yake kabambe inayoitwa "Wese Ndio Mchongo" inayotoa fursa kwa wateja wake kote nchini kujaziwa mafuta kwenye vyombo vyao usafiri.

Hatua hiyo ni zawadi kwa wateja wa shirika hilo katika kuadhimisha ya miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara pamoja na miaka 58 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa kampeni hiyo ya miezi mitatu uliofanyika jijini Dar es Salaam katikati ya wiki Mkurugenzi wa Biashara na Uwekezaji wa Shirika hilo. Mohammedi Ameir, alisema kampeni hiyo inawalenga wateja wa bima kubwa ya vyombo vya moto ambapo kila mteja atayekata bima hiyo atakuwa kwenye nafasi ya kujipatia mafuta kwa ajili ya chombo chake cha usafiri.

"Shirika la Bima Zanzibar ni shirika ambalo linawateja wengi kutoka pande zote kwa maana ya Tanzania Bara na Zanzibar na siku zote tumekuwa karibu zaidi na wateja wetu. Kwa kuliona hilo tumeona katika kipindi hiki ambacho tunasherehekea maadhimisho haya muhimu kitaifa kwa pande zote mbili ni vema tuje na zawadi hii kwa wateja wetu.

"Pamoja na maadhimisho haya tunaamini washindi wetu wataweza kutumia zawadi hii ya mafuta kuokoa fedha ambayo wataitumia kwenye matumizi yao mengine ya mwisho wa mwaka ambao huwa unaambatana na sikukuu pamoja na mahitaji ya shule kwa watoto," alisema.

Mkuu wa Kituo cha Mauzo ZIC tawi Posta Mpya jijini Dar es Salaam, Amina Mohammed, alisema ili mteja aingie katika droo ya kujaziwa mafuta ni lazima afike katika ofisi za shirika hilo zilizopo kote nchini kwa ajili ya kukata bima kubwa ambayo itamwezesha yeye kupata bahati ya kujaziwa mafuta kuanzia lita tatu (3) hadi lita 100.

"Kitakachoamua kiasi cha mafuta anachostahili kupatiwa mteja ni bahati yake katika kuchagua kimpira kidogo (ball) chenye karatasi ndani iliyoandikwa kiasi cha mafuta aliyoshinda ili aweze kupatiwa mafuta yake kupitia vituo mbalimbali vya mafuta kokote alipo nchini," alisema.

Kampeni hiyo itadumu kwa muda wa miezi mitatu, ikilenga kuwafikia wateja wote wa Shirika la Bima Zanzibar waliopo Tanzania nzima, ikiwa na kauli mbiu "Wese Ndio Mchongo, Kata Bima Tukajaze Wese".

# Wathamini waonywa kuhusu udanganyifu

**Na Munir Shemweta,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amewataka wathamini nchini kuepuka udanganyifu, maarufu kama Tegesha, wakati wa kufanya uthamini wa majengo na mali kwa ajili ya ulipaji fidia.

Dk. Mabula alitoa kauli hiyo juzi wakati akifunga Mkutano Mkuu wa Pili wa Mwaka wa Wathamini uliofanyika mkoani mjini hapa.

Alisema ni vizuri wathamini wakati wa kutekeleza majukumu yao, wakawa makini na kuhakikisha wanaepuka udanganyifu wa aina yoyote ukiwamo ule wa Tegesha, alisema ulijitokeza katika uthamini uliofanyika mgodi wa North Mara-Nyamongo.

"Kuweni makini wakati wote mnapokuwa uwandani na kuepuka udanganyifu kama uliofanyika North Mara-Nyamongo. Mmea unapandwa usiku na unafanyiwa uthamini na kusababisha serikali kupoteza fedha na mchezo huu umefanyika sana. Wote mnajua yaliyotokea, hivyo tusingependa yajirudie," alisema Dk. Mabula.

Aliwataka watumishi wote wa sekta ya ardhi na fedha wanaofanya kazi na wathamini kuwa waaminifu ili wasiwashawishi wathamini kujiingiza kazi zisizozingatia uadilifu, sheria, kanuni na taratibu. Alisema ukiukwaji maadili unasababisha sintofahamu au malalamiko yasiyo ya lazima kutoka kwa wateja.

Dk. Mabula aliitaka Bodi ya Usajili Wathamini kupunguza vikwazo vya usajili kwa kuitaka kuharakisha usajili kwa wale wote waliotimiza vigezo. Alisema ucheleweshaji wowote unaofanyika unawakosesha haki katika utumishi ikiwa ni pamoja na kupanda vyeo.

Kwa sasa zaidi ya wathamini 200 waliopewa mafunzo ya uthamini wanafanya mitihani ya usajili ya bodi kwa ngazi mbalimbali. Baadhi yao wanakamilisha makala za utafiti ili kupata usajili kamili wakiwamo wathamini wa ofisi za mikoa na halmashauri.

Kupitia mkutano huo, Naibu Waziri aliitaka bodi kusimamia kwa karibu kampuni zote za uthamini ili zifanye kazi kwa weledi huku akisisitiza kesi zinazopelekwa kwenye bodi na wizara kutolewa ufumbuzi mapema.

Kuhusu Sh. bilioni 50 zilizotolewa na serikali kupitia Wizara ya Ardhi kwa ajili ya mradi wa Kupanga, Kipima na Kumilikisha (KKK) katika halmashauri mbalimbali nchini, Dk. Mabula aliwataka wathamini kuhakikisha wanatimiza wajibu wao kwa kuzingatia maadili wakati wote wa kutekeleza mradi huo katika halmashauri.

Kaimu Msajili wa Bodi ya Wathamini, Joseph Shewiyo, alimwahidi Naibu Waziri kuwa bodi yake itahakikisha inasimamia maadili kwa wathamini pamoja na kusimamia kampuni zote za uthamini ili yafanye kazi kwa weledi.



Ukurasa 12

Wasira asimulia uzalendo ulivyozama kwa mabosi enzi kazini hadi 'shuleni




Ukurasa 13

Chifu Hangaya, nahisi ile 'coma' sasa imekomaa



Ukurasa 14

**KAPTENI LIGORA ASIMULIA:**

**Nakumbuka vizuri tulivyousherehekea siku mbili kijijini, ukaniajiri jeshini hadi chama**

# BUFE

IJUMAA DESEMBA 10, 2021
Nipashe

**MIAKA 60 YA UHURU**

LT. KANALI MSTAAFU MAKELELE:

# Naikumbuka siku niliyofurahi hadi nikalia, kila kaya mtaani ilikesha

• Mvua ilinyesha wakaamini 'baraka za Mungu' • Mifugo ilichinjwa, pombe kangara...'usiseme' • Bendi kutoka Uganda; tuliwazomea Wazungu • Bibi mkongwe akumbuka tabasamu la siku hiyo

**Na Anthony Gervas**, MWANZA

MWAKA 1961 ndiyo Tanganyika ilipata Uhuru chini ya uongozi wa Mwalimu Julius Nyerere, aliyekuwa mstari wa mbele kupigania uhuru na baada ya mafanikio akawa Waziri Mkuu, kisha Rais baada ya mwaka mmoja.

Mwalimu Nyerere na wenzake aliyofuatana nao aliendesha harakati za kuikomboa Tanganyika kutoka mikononi mwa wakoloni Waingereza, ndiyo mzizi kila tarehe kama ya jana kumesherehekewa Siku ya Uhuru kitaifa.

Siku wakoloni wakikabidhi serikali kwa Watanganyika, mkoani Mwanza nako wako mashuhuda wa namna bendera ya serikali yao iliteremshwa na kupandishwa ya Tanganyika. Kama iliyotokea huko Lindi na kwingineko, mashuhuda wengi walipigwa na butwaa, hawakuamini.

Inaelezwa, mkoa wa Mwanza uligubikwa na vifijo, nderemo nyimbo za furaha ukiwamo wa taifa, vigelegele baada tu ya kupandishwa bendera hiyo ya Tanganyika na kushushwa ya wakoloni, chini ya utawala wa Malkia Elizabeth.

Ndiyo maana kila mwaka Desemba 9, ni siku ya kusherehekea kumbukumbu ya Tanganyika kupata uhuru na leo inatimiza miongo sita kamili.

**MWANZA ILIVYOKUWA**

Luteni Kanali Mstaafu Pius Makelele, mzaliwa wa mkoani Mwanza, kijana wa wakati huo na babu wa sasa, ana simulizi namna tukio hilo lilivyomfikia akiwa kijana mbichi wa umri wa miaka 22, mwanafunzi wa kidato cha tatu katika Shule ya Sekondari Seminari Nyegezi Mwanza.

"Wakati bendera ya serikali ya Uingereza ikiteremshwa na kupandishwa bendera ya serikali ya Tanganyika ilikuwa majira ya saa sita usiku. Nilifurahi mpaka nililia machozi," anasimulia, pasipo kujua baadaye angekuwa afande jeshini.


Luteni Kanali Mstaafu Makelele, anayejitambulisha kuwa mzaliwa wa Bugando jijini hapo, anasema ni tukio lililomkuta akiwa likizo nyumbani.

Anasema aliwaona askari polisi wakiwa na sare zao, kaptula za kaki na mashati ya aina hiyo wakiwa kwenye 'paredi' (gwaride) wakishiriki tukio la kushusha na kupandisha bendera ya serikali ya Tanganyika.

Baada ya kumaliza hatua hiyo, wimbo wa taifa uliimbwa na Polisi na wakapiga mafataki kuashiria Watanganyika wameshapata uhuru wao, bendi na ngoma kutoka nchini Uganda zilikuwapo wakicheza pamoja na wananchi.

"Watu walifurahia kupata uhuru, wengine walikuwa wakiwazomea Wazungu kuondoka, kutokana na kuchoshwa na ubaguzi, manyanyaso yao, kila kaya walikesha wakisherehekea hadi majumbani mwao wakila na wakinywa pombe za kienyeji.

Afande huyo mstaafu, anakumbuka namna walivyokunywa pombe za kienyeji za aina mbalimbali, akizitaja baadhi ni kangara, mapuya na gongo na watu wachache wenye uwezo walikunywa bia.



Luteni Kanali Mstaafu Pius Makelele, akiwa nyumbani kwake na wajukuu zake jijini Mwanza. **PICHA: ANTHONY GERVAS**

Pia anasema, ni tukio lililoendana na uchinjaji ng'ombe, mbuzi, kondoo kufurahia Uhuru.

**MAISHA YA UKOLONI**

Luteni Kanali Makelele anasimulia kwamba kipindi hicho wananchi wengi mkoa wa Mwanza walikuwa wakiishi nyumba za udongo zilizoezekwa nyasi.

Wakati huo wa ukoloni, anaisimulia Nipashe kwamba, katika zama kabla ya uhuru, kulikuwapo jamii ya Wazungu, Wahindi na Waarabu wachache, akilalamika walikuwa na tabia za kibaguzi wakiwanyanyasa wao wenyeji mkoani.

Watu chache wenye uwezo walijenga nyumba za matofali ya tope na kuezeka kwa 'mabati ya madebe' ikiwamo hasa jamii ya weupe, huku asilimia kubwa ya wenyeji nyumba zao ziliezekwa kwa nyasi, huku wakishi gizani kwa kukosa huduma ya umeme.

Namna wanavyoishi, Mzee Makelele anasema ambao walikuwa na uwezo kiasi wa kiuchumi, kwa kiasi kikubwa wageni walitumia vyanzo vya umeme kama majenereta makubwa kuwasha umeme kupitia kampuni anayoitaja ya Daresco kutoka mkoani Dar es Salaam, lakini wananchi wengi walitumia taa za chemli.

Baada ya uhuru, anasema serikali ilitangaza marufuku kwa mtu yeyote kuvaa nguo nyeusi aina ya kaniki kwamba zinadhalilisha na kushusha heshima ya uhuru.

Kwa kiasi kikubwa, kaniki ilikuwa vazi jeusi lililovaliwa na kinamama na wengi hasa walitumia kwenda shamba, ikitajwa kuwa na uwezo mkubwa kuhimili msukosuko kama ile ilivyo khaki kwa wanaume.

Afande huyo mzaliwa wa mwaka 1938, anasimulia kadri siku zilivyokuwa zinasonga mbele, serikali iliwapimia viwanja wananchi eneo la Mabatini na kupiga marufuku eneo hilo kujengwa nyumba za nyasi, ikitaka kila mtu kujenga nyumba ya mabati ya madebe, ndiyo kukazaliwa jina la Mabatini.

**INAENDELEA UK.12**

MIAKA 60 YA UHURU

# Wasira asimulia uzalendo ulivyozama kwa mabosi enzi kazini hadi shuleni

## • Akumbuka Mara 5000 walijitolea Vita vya Kagera

Na Romana Mallya

STEPHEN Wasira ni waziri mstaafu aliyehudumu katika awamu tatu za serikali; ya kwanza, pili na ya nne, sasa ni Mwenyekiti wa Chuo cha Kumbukumbu cha Mwalimu Nyerere (MNMA).

Tarehe 19 mwezi uliopita katika Kampasi ya Kigamboni, Dar es Salaam kuliandaliwa kongamano la Maadhimisho ya Miaka 60 ya Uhuru wa nchi ikiwa na mada "Uongozi na Maadili katika Miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Tanganyika."

Ni kongamano lililohudhuriwa na wengi wakiwamo wanafunzi wa shule za msingi na vyuo. Baada ya uwasilisho wake mtoa mada Wasira, ndio akaulizwa swali lililohitaji ulinganishi kutumia uzoefu wake, kati ya zama alizotumikia na sasa.

### ATIRIRIKA SIMULIZI

Wasira anaanika uzoefu na ufahamu wa kutosha walikotoka kuanzia zama chini ya Rais Julius Nyerere, akianza kuainisha teknolojia wakati wa ujana wao hakukuwapo mtandao wa simu za mkononi.

"Wakati ule Mwalimu (Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere) wakati anaongoza tulikuwa na njia mbili za kufikia jamii. Moja ya Redio Tanzania Dar es Salaam, kabla iliitwa Sauti ya Dar es Salaam, magazeti Daily News na Uhuru na kabla ya Uhuru yalikuwapo Mwananchi," anasimulia.

Anaendelea: "Kwanza viongozi walifunzwa ndipo wakaenda kuongoza. Pili, mawasiliano ya viongozi na jamii yalikuwa yanapitia vyombo ambavyo havikuwa vingi kama ilivyo sasa.

"Unaweza kumsikiliza daktari pale (mhadhiri) anakueleza, unaenda 'kuperuzi' mtandaoni unataka 'google' ikupe tafsiri ya yale uliyoelezwa na daktari, baada ya 'kuperuzi' unaona mwalimu amekosea kwa sababu 'google' inasema tofauti na mwalimu. Hii ni tofauti kubwa namna mawasiliano yanavyowafikia."

Wasira anataja la pili, zamani walipohitimu masomo walienda kushika nyadhifa za juu kama mkuu wa wilaya, huku mtu anachokifikiria ni kuingiza aliyofunzwa kwa jamii.


"Siku hizi sitaki kuwatania, naona vijana wapo wengi. Lakini, mawazo yamebadilika kidogo. Mtu akiajiriwa zamani anataka kuona ufanisi wa kazi alizopewa. Siku hizi mtu akiajiriwa, kwanza anataka nyumba katika mshahara wa kwanza.

"Halafu anataka anunue gari kabla ya mshahara wa kwanza haujaja. Sasa vipaumbele vinapingana, mtu anafikiria nitapata wapi fedha ya kununua gari hapo, ndipo kipaumbele vinakinzana ndipo ubadhirifu unapokuja.

"Sasa hapo anaona cha kufanya ni kudokoa kwenye meza aliyopewa. Waswahili wana maneno wanasema kila mbuzi anakula kwa urefu wa kamba yake. Kusema kweli kumekuwapo matatizo.

Wasira anatumia mfano wapo watendaji na wenyeviti wa vijiji na mitaa wanaoteuliwa na kwenda kufanya kazi bila ya mafunzo.

Anafafanua: "Hata wewe ukiwauliza hili swali nao waseme huko waliko, hawawezi kusema, watakushangaa uliyeuliza swali na watu ambao hawajui mara nyingi wanakuwa wakali sana ukiwauliza, kwa sababu anaona unataka kuikosoa mamlaka."



Mwenyekiti wa Chuo cha Kumbukumbu cha Mwalimu Nyerere (MNMA), Stephen Wasira, akimkaribisha Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, katika halfa ya ufunguzi wa Kongamano la Miaka 60 ya Uhuru wa nchi. Kando kwake, ni Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Pro. Joyce Ndalichako. PICHA ZOTE: MTANDAO

Mkongwe huyo anaendelea: "Tofauti ambazo zipo, moja elimu haijatusaidia katika jambo hili. Mfano alipokuwapo Rais John Magufuli aliposema tuanze kufundisha somo la historia, sijui kama tumeanza? Lakini, suala lilikuwa unawezaje kumfanya mtu awe mzalendo asiyeijua nchi yake? Uzalendo ni kuijua kwanza nchi yako.

"Pili, ni kuipenda. Sasa unaipenda nchi usiyojua, unaipendaje? Utapendaje usichokijua? Matatizo yapo kwa nchi, tuanze kuyapeleka mafunzo yetu kuanzia shule za msingi, tuanze kujenga uzalendo wa kweli unaowafanya watu kujua nchi yao na ukiijua utakuwa na mapenzi nayo, uzalendo ni kujitoa muhanga."

Anatoa mfano wa vijana waliopo jeshini akiuliza hadhira ya iliyohudhuria kongamano, kama wanadhani wenzao waliko huko ni kwa ajili ya mshahara mkubwa?

"Kama kuna mshahara mkubwa, nenda basi wewe kama shughuli yako ni mshahara tu uende kule tukakufundishe uchukue bunduki," anawaambia kwa lugha ya mfano, akiendelea: "Wanapigana kwa sababu wamepikwa, wamejua nchi yao na wanajua uchungu wa nchi kudhulumiwa."

Wasira anasema alipokuwa Mkuu wa Mkoa wa Mara aliwaandikisha wana mgambo wapiganaji wa Vita Kuu vya Pili kwenda kupigana wakati wa vita dhidi ya Idd Amin.

"Nilikuwa na daktari wangu ambaye ndiye alikuwa akiwapima. Tukaenda kijiji kimoja kule Tarime, wakati anawapima mmoja akamwambia shinikizo la damu lipo juu sana. Yule aliyepimwa alipoambiwa akasema hapana, nimekuja hapa kwa haraka, ndiyo maana imepanda. Alitoa hoja hiyo ili daktari amwandikie yupo sawa aende kupigana.

"Daktari akaniuliza, 'Hawa watu wa huku wakoje, huyu anataka nimpeleke vitani aende kufa?' Nikamwambia haendi kufa, anaenda kupigana. Ingekuwa kufa, hakuna ambaye angekwenda, tunawafundisha kupigana, kujihami, kuua na kuhakikisha wao hawafi, lakini kinachowapeleka kule ni uzalendo," Wasira aliwaambia wanafunzi.

Mkongwe huyo anatoa mfano mwingine wa kaka yake aliyekuwa mtu mzima, naye wakati huo alipigana Vita Kuu vya pili. Wasira aendeleza simulizi yake:

"Nilimwambia kaka wewe ni mtu mzima huwezi kwenda, akasema, 'Unasemaje? Nchi imetekwa unasemaje?' Tukawa tunawapa posho akasema, hataki fedha anataka bunduki aende kupigana.

"Ingekuwa sasa mngesema fedha kiasi gani kwanza, si mnataka tofauti. Ingekuwa sasa mngeuliza mnatulipa shilingi ngapi? Mnatulipa malipo ya awali kiasi gani? Hawakutaka fedha walitaka bunduki na chakula ili wapate nguvu.

"Wa namna hii walikwenda wengi nakumbuka 5,000 tena wengine watu wazima. Uzalendo ni mapenzi ya mtu kwa nchi yake. Huwezi kupenda nchi usiyoijua, tuijue Tanzania tujue historia yake ituongoze katika kuipenda."

Anawakumbusha kuwa waliopigania uhuru wa nchi wangekuwa watu wanaopenda fedha za haraka, Mwalimu Nyerere asingeacha ualimu wake, halafu aende Butiama bila ya mshahara.

"Akawa anatoka Pugu kwa miguu na ana Masters (Shahada ya Uzamili) kuja Lumumba (katikati ya jiji Dar es Salaam) kushirikiana na wazee wa wakati ule kudai uhuru wa Tanganyika angeweza kusema kwa nini?"

Baada ya hoja hiyo 'kigongo' akaendelea apeleke Pugu halafu mje kwa miguu? Ninadhani nimeeleza tofauti za nyakati, tofauti za misimamo zinazotokana na mfumo wa elimu tunaoutoa.

"Hili ni jambo ambalo linazungumzika. Tuzungumze hivi kweli elimu tunayotoa inawafanya vijana waijue vizuri Tanzania, waipende na wawe tayari kuitetea.

"Wengine wanaweza kuuliza upo wapi uhusiano kati ya uadilifu na uzalendo. Hivi wewe kama unaiba tu, unakula rushwa, unaweza kuunganisha watu kuleta amani, itoke wapi?

"Wewe mwenyewe ni chanzo cha uvunjivu wa amani, wengine hawaelewi rushwa inavyoathiri jamii, haya ndiyo mambo ya kujifunza. Tunapojifunza, tujiulize tunataka kuipeleka nchi yetu wapi?"

### TUENDAKO JE?

Huku akiwataka vijana kujifunza na kuhoji mengi waidhinishe uzalendo wao. Anaendelea: "Msibaki mmenyamaza tu na mkafikiri kunyamaza na kufanya unafiki kuwa ndio uzalendo. Uzalendo wa namna hiyo hauna maana, tena siutaki kabisa, uzalendo wa unafiki? Hapana! Ndiyo maana wengine tumekuwa tunahoji.

"Nimefanya kazi na Mwalimu Julius Nyerere na watu wengine walifikiri Mwalimu hawezi kuulizwa, lakini siyo kweli. Kuna siku nilimuuliza" anabainisha mstaafu huyo, akiwataka vijana waendelee kujifunza maadili na historia ya nchi hata kama ni kwenye mitandao, wasome na kuchuja.

"Tumewajengea nchi, tunaweza tukawa hatujafikia lengo, lakini tumejenga chini ya uongozi Mwalimu Nyerere kuijenga nchi yenye umoja, kubwa mnaweza kutukosoa unayotafakari kwa miaka 60, lakini bado tutakwambia tumejenga nchi," anasema.

Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Shadrack Mwakalila, anahitimisha kwa kufafanua majukumu yao hivi sasa wanafundisha taaluma mbalimbali; uongozi, maadili, uzalendo na utaifa, sambamba na utafiti, pia kuna utaalamu.

## Naikumbuka siku niliyofurahi hadi nikalia, kila kaya mtaani ilikesha

INATOKA UK.11

### MVUA ZA UHURU

Tukio la uhuru analisimulia, liliendana na mvua iliyonyesha hata watu wengi waliamini 'Ni kweli Mwalimu Julius Nyerere ameingia madarakani na baraka za Mungu."

Wananchi wakaliunga mkono tukio la mvua hizo wakilima mazao kama mpunga, mahindi, viazi na mihogo na mwaka huo haikushuhudiwa njaa.

Mvua hiyo iliyonyesha mjini hapa miaka hiyo 60 iliyopita ilizamisha ofisi kuu ya TANU Mwanza katika Mtaa wa Seleman, sambamba na mitaa ya Makongoro, Mwaloni hadi Nyakahoja walikoishi zaidi jamii ya Wazungu na Wahindi.

### KABLA YA UHURU

Mzee Makelele anarejea kumbukumbu kabla ya uhuru mkoani Mwanza, makao makuu ya jimbo Kanda ya Ziwa, Mwalimu Nyerere tangu aanze rasmi vuguvugu zake za wazi kutafuta hasa mwaka 1955, alionekana kuwa na kasi ya ajabu akawa anasifika hadi shuleni, hali iliyowapa hata mshangao jumuiya ya Wakoloni.

Anasimulia wakati mwalimu Nyerere akidai uhuru Wazungu, Wahindi na Waarabu walimpinga vikali, wakiuliza kwa kejeli "kwanini Watanganyika wanataka kujitawala, wakati hawana uwezo hata kutengeneza sindano ya mikono?"

Mzee huyo anakumbuka namna Nyerere alivyopigwa marufuku kufanya mikutano yake ya hadhara kwa wananchi mkoa wa Mwanza, kulikokuwa makao makuu ya Chama Kikuu cha Ushirika cha Wakulima wa Zao la Pamba cha Wasukuma (Victoria Federation Union) (V.F.U), Meneja wake mwanzilishi akiwa marehemu Paul Bomani.

Kutokana na kupigwa vita hivyo, anasema Nyerere alikuwa mjanja kwa kubuni mbinu mbadala ya kufanya kampeni zake kimyakimya, hali iliyowapa ugumu Wazungu kutafsiri au kugundua nyendo zake.

### BIBI AFUNGUKA

Bibi Justa Lucas, ni mkazi na mzaliwa wa jijini Mwanza, anaelezea kilichojiri wakati wa uhuru, kwamba kwenye makazi ya watu yalikuwa mbali kati ya kaya moja hadi nyingine na hakukuwa kumepangwa na serikali.

Justa, mzaliwa wa mtaa wa Uhuru ambao wakati huo uliitwa Mtaa wa Shabaha na sasa anaishi Mtaa wa Unguja, anasema kulikuwapo mashamba mengi na majaruba ambayo wakulima walilima mazao mbalimbali kama mpunga, mihogo na viazi.

"Wakati wa Uhuru kulikuwa na mtaa mmoja tu maarufu tuliokuwa tukiishi unaitwa Mtaa wa Shabaha, ambao kwa sasa unaitwa Uhuru," anasimulia Justa, akisema palikuwapo maduka mengi ya Wahindi na Waarabu wachahe, lakini watu weusi hawakuwa na maduka.

Anakumbuka maisha ya wakati huo uliopita wakisema mahitaji mengi waliyapata madukani kwa waliowaita wakati ule 'Baniani.'.

### SIKU YA UHURU

"Siku ya kupatikana uhuru katika mkoa wa Mwanza nilikuwa binti mwenye umri takribani miaka 15. Nilizaliwa mwaka 1946, niliona bendera ya Waingereza ikishushwa na kupandishwa ya serikali ya Tanganyika. Taa zilizimwa, tulifurahi mno siku hiyo," anasimulia Bibi Justa.


Anasema siku hiyo walivaa vitenge vilivyoandikwa 'Uhuru' vifijo na nderemo zilisikika kila mtu aliimba nyimbo za kufurahia, walikula na kunywa wakiamini ukombozi wao umetimia.

Hata hivyo, anakumbuka miundombinu ya umeme hai-

INAENDELEA UK.14

## TAFAKURI YA MLALAHOI

### Chifu Hangaya, nahisi ile 'coma' sasa imekomaa




TUKO mwisho wa mwaka. Kila mmoja anawaza lake. Wapo wawazao sikukuu zijazo, lakini kubwa wanawaza ada za shule mwakani zitapatikana patikanaje. Wamachinga wanahaha kuona ni jinsi gani ugali utaingia kinywani.

Wapo wanaowaza Desemba mwaka jana ilikuwaje na wanatazama hata wakilinganisha Desemba hii na ile. Wanawaza Desemba tangu zama za Magu na leo Desemba ya Chifu Hangaya.

Lakini, mimi mwenzenu siwazii hayo kwa sababu jana na leo kwangu ni yale yale tu na nadhani hata kesho kama mwendo ni huu, yatabaki kuwa yaleyale, nami kuendelea kuwa yuleyule tu. Kinachonijia na kukiwaza ni 'coma' ya Mama!

Wakati 'coma' hiyo ikisumbua kichwa changu, narudisha mawazo nyuma, nikiangalia kinachoendelea leo huku na kule.

Naona kuna vitu vinateka kabisa akili zetu na kuacha kufikiria mengine ila kuwaza Watanzania tumejikita huko. Hapana sababu ya kujiuliza kwanini, ila ni kutokana na matukio yaliyopita katika jamii na nani aliyeyafanya na yaliigusa vipi jamii na mtu mmoja mmoja.

Ndiyo sababu watu wanashinda mitandaoni, kwenye magazeti, redio, vijitiviii na tivii.

Nakumbuka mabosi fulani wa kiserikali huko nyuma waliwahi kufanya mambo fulani yasiyoeleweka eleweka hivi! Yakafurahisha na kukera wengine. Yakagusa na kufikirisha wengine. Wapo walioshangilia kwa makofi na vigelegele, lakini wengine wakapatwa kichefuchefu.

Nakumbuka mmoja siku fulani akamfokea mkurugenzi wake mbele ya kadamnasi wakiwamo wadogo zake kikazi, eti kwanini kachelewa kwenye jambo lake. Akafoka sana, lakini leo aliyekaripiwa yuko juu ya mfokaji wa awali (kicheko).



NA JOSEPH KULANGWA
+255 713 410008
jkulangwa@yahoo.com

Mzito mwingine naye hivyo hivyo, siku moja mkutanoni katika ukumbi fulani hivi nchini, akawa anamkemea bosi msaidizi wake aliyekuwa anajieleza.

Alimkemea mithili ya mzazi kwa mwanawe. Leo bosi mfokaji sijui yuko wapi na aliyekemewa amekalia kiti fulani cha kitaifa akitumika (kicheko).

Ndiyo sababu nawaza, hivi wakikuta na hawa mahali fulani sijuio itabeba taswira gani? Tutacheka tu na kuyaacha hapo, kwa sababu Wabongo wengi tuna tabia ya kumwachia Mungu tunapoona yametushinda.

Lakini, ni juzi yupo fulani yupo bosi ngazi fulani alimkemea mtumishi wa umma fulani wa umma hadharani, eti akitaka asijieleze ila amsikilize yeye tu. "Wewe unapaswa kunisikiliza mimi, si nikusikilize wewe…!" Utadhani Mungu! (kicheko).

Nimewaza huko, kwa sababu naona Chifu Hangaya bado kuna watu wanamchezea akili, bado kuna watu wanamdanganya kuwa wanachapa kazi, lakini kumbe ni mbwembwe na tambo za bure tu, wakidhani haoni. Ye alishasema msione macho yake yako vile, yanaona ile mbaya.

Na alishasema hata siku moja hamtamwona hadharani kutukana au kukaripia mtu, ila kalamu yake ndiyo silaha yake. Utalimwa na utajikuta pembeni unakuwa ndugu mtazamaji au ndugu msikilizaji tu!

Si siri, kuna maeneo makubwa kwa umuhimu na majukumu kitaifa, mambo hayaendi kama inavyotakiwa, kama anavyotaka Chifu Hangaya.

Kuna wenye dhamana zao wanazurura tu ki-Vasco da Gama, kumwonyesha Chifu Hangaya kuwa wanatenda inavyotakiwa, lakini kumbe hakuna kitu.

Kama walivyofanya enzi zilizopita kumsifia mkuu kwa kutaja majina yake manne na kumsingizia kwa kila zuri, ili waendelee kutetea matumbo, ndivyo walivyo hata leo wakimsifia Chifu Hangaya kwa majina yake matatu. Lakini ni kwambie, ni anakuangalieni tu kwa macho yake hayo, ohooo!

Kama mu wabunifu kweli, mmeona tumepitia kipindi kigumu cha ukame, hakuna maji hakuna umeme, haya mmekuja na ubunifu gani sasa?

Mvua zimeanza watu wametulia na kusingizia maombi, ukame ukija tena wanaanza kuhaha bila suluhu. Mnataka Binti Suluhu akupeni suluhu, nyie mwafanya nini?

Mama Chifu Hangaya, hebu funua ukurasa ule pale ulipoachia ile 'coma' ili uendelee na ulichokuwa ukikiandika, naona kama 'coma' imekomaa hapo muda sasa, mpaka tutasahau kuwa kuna watu wanastahili sasa kuwa ndugu watazamajina wasikilizaji! Alamsiki!

KAPTENI LIGORA ASIMULIA:

# Nakumbuka vizuri tulivyousherehekea siku 2 kijijini, ukaniajiri jeshi hadi chama

**Na Sabato Kasika**

- 'Baibai' wasiolipa kodi kuota moto mchana
- Shule mpya kijijini, ikamfaulisha peke yake



Mohamed Ligora (kushoto), akiwa na wazee wenzake wa Jiji la Dar es Salaam, walipotembelea Ofisi za Idara ya Habari Maelezo. **PICHA: MAKTABA**

UKIMWONA leo ana wajihi wote wa uzee. Lakini ukimtafiti kwa kina, unagundua yu imara kuanzia ngazi ya mwonekano katika sura yote inayotetea wasifu wake, Kapteni mstaafu wa Jeshi la Wananchi Tanzania, Mzee Mohamed Ligola.

Naam! Hebu thubutu kumdadisi chochote cha kihistoria katika nchi hii kuanzia zama za mkoloni, siku hiyo tunayoishangilia leo na mtiririko wote wa kiserikali, pia kihistoria baada ya hapo.

Katika hatua yote amekuwa na hisa ya moja kwa moja kushiriki katika sura ya kitaifa, hata nathubutu tena kumtania kichwani ana mtandao wa 'google'.

Katika mazungumzo yake na Nipashe wiki hii, anasimulia namna yeye ni miongoni mwa waliokuwa vijana wadogo wakati huo Tanganyika inapata uhuru, akiwa kijiji kwao Chunyu, wilayani Ruangwa mkoani Lindi ilikuwa siku ya kicheko kilichopitiliza.

Anasema siku hiyo ya uhuru Desemba 9, mwaka 1961, alishuhudia watu wakisherehekea kwa siku mbili wakila na kunywa pombe za kienyeji, hata kucheza ngoma mbalimbali za asili ikiwamo anayoitaja kwa jina la 'Likundumbwi'.

Ligola ambaye ni mahiri wa kufafanua hoja, anadokeza kutokana na namna utawala wa kiloloni ulivyojikita nchini, bado walikuwa wazito kuamini dhana ya ukoloni umefikia 'kwa heri' ya kudumu hata walianza kwa kusita, kbala ya imani kamili kuwaingia na wakaanza kutoka nje ya nyumba zao kushangilia.

### KULIKONI AKASITA?

Kapteni Ligola anasimulia hatua ya wao kusita, ilitokana na mateso waliopata katika zama hizo za ukoloni walipokuwa wakishindwa kulipa kodi, akikumbushia ya shilingi tano kwa mwaka, ambayo ilikuwa kiasi kikubwa sana cha pesa.

"Ni hivi, babu yangu mzaa mama, Sheikh Said Kianga, Jumbe wa Kijiji cha Chunyu, cheo ambacho kwa sasa kinaitwa Mwenyekiti wa Kijiji, alikuwa akikamata wasiolipa kodi na kuwapa adhabu ya kuota moto wakati wa jua kali.

Anasema, alifanya hivyo kwa maelekezo ya wakoloni, ingawa mwenyewe alikuwa hapendi. Ni hali iliyosababisha watu wamwogope na kwamba hata alipotangaza nchi imekuwa huru, bado walisita kwanza kuwapo mabadiliko hayo.

"Yaani ni kwamba waliokuwa wanashindwa kulipa kodi, walitakiwa kupeleka kuni kwa jumbe zikawashwa huku wakiamriwa kuota moto mchana kweupe kwa mwezi mmoja, adhabu ambayo iliwaumiza sana," anasema.

Anasimulia akiwa na utetezi kwa babu yake kwamba kamwe hakuipenda adhabu hiyo na akabuni mbinu ya kuwatetea wasitaabike dhidi ya madhila hayo ya kikoloni.

Ili kuhakikisha anafanikisha yote, Jumbe (Mwenyekiti) Mzee Kianga, alitumia staili ya kumtuma mjukuu wake (Kapteni Ligola) kwenda kukaa njiapanda kuangalia kama askari wa mkoloni wanakuja na inapotokea Ligola anapiga mluzi kama ishara ili watu wende kuota moto.

"Wakati huo nilikuwa ninasoma darasa la pili nikishuhudia hayo yote. Siku ya uhuru babu na wasaidizi wake walipita usiku na kutangazia wananchi kuwa Tanganyika imekuwa huru kutoka kwa wakoloni," anasimulia.

Anasimulia, mbali na kusherehekea ya tukio hilo lililojiri kwa siku mbili mfululizo, kulikuwa na hali ya kushangaza hata ya ndege aliowataja kwa jina la 'mabaranguro' walionekana wakiruka kwa wingi siku hiyo angani na kuwafanya watu washangae kwa kuwa haikuwa hali ya kawaida.

### BAADA YA UHURU

Kapteni Mstaafu Ligola, anasimulia maisha mapya baada ya Tanganyika huru, kwamba mara moja walishuhudia kulijengwa shule katika kijiji cha Matambarare, ambako alipelekwa na wazazi wake kusoma.

Huko alifaulu peke yake kwenda kujiunga darasa la tano katika shule iitwayo Ziwani Middle School ya Lindi, alikohitimu darasa la nane. Hapo anaendelea "Yaani ni kwamba, kabla ya uhuru, kulikuwa na 'kishule' kimoja kijijini ambacho tulikuwa tunasoma na kurudiarudia darasa la pili, kwa sababu kilikuwa hakiendelei zaidi ya hapo," anasema.

Kapteni Ligola anasema, baada ya kuhitimu darasa la nane alifanya kazi ya ukarani katika Chama cha Ushirika cha Kijiji cha Chunyu, baadaye mwaka 1968 akaenda masomoni nchini Israel, kwa mwaka mmoja.

Anasema baadaye alienda mafunzoni, katika chuo cha kijeshi Monduli maalumu kwa yaliyowahusu. Arusha inayohusu makada wa TANU wakati huo na kwamba kozi yao iliendeshwa katika mahema chuoni hapo.

"Ilikuwa ni mwaka 1975, kamanda wetu alikuwa Hans Kitine, nilikuwa pamoja na Moses Nnauye, miye nilishughulikia UNITA, Nnauye alishughulika na MPLA, ni vyama vya siasa vya Angola," anasema.

Ligola anasimulia, baada ya kutoka Monduli, alishaiva kitaaluma kwa wadhifa wa ofisa wa jeshi na baadaye mwaka 1978, akapata kozi anayoiita ya 'Kombania' jeshini, kisha akaenda vitani katika vita ya nchini Uganda. Aliporejea, ndio alitunikiwa cheo cha kapteni.

### ALIVYOTUMIKIA UMMA

"Nilistaafu rasmi jeshini mwaka 1992, nikateuliwa na CCM kuwa Katibu wa Chama Mkoa wa Ruvuma, baadaye nikahamishiwa mkoa wa Lindi, nikastaafu nafasi hiyo (Katibu wa Mkoa) mwaka 2003 nikiwa Mkoa wa Dar es Salaam," anaeleza.

Mkongwe huyo wa siasa, anasema baada ya kustaafu ukatibu wa CCM Mkoa wa Dar es Salaam, alipelekwa katika Ofisi Ndogo ya CCM Lumumba kuwa Mkuu wa Utawala hadi mwaka 2009 alipostaafu. Pia anakumbuka operesheni ya kuchana nguo fupi na za kubana kwa kinamama, jijini Dar es Salaam mwanzoni mwa miaka ya 70, wakati huo akiwa kijana wa TANU, nakumbuka jinsi alivyoshiriki kikamilifu.

Anasema wote waliokutwa wamevaa gauni fupi au suruali za kubana, walichaniwa kwa lengo la kusimamia maadili mema ndani ya jamii na anajisifu walifanikiwa kwa kiasi kikubwa.

"Kwa wale wanaovaa nguo fupi na za kubana, wajue kuwa zilikuwapo tangu zamani. Tulizidhibiti ili kulinda maadili mema, lakini sasa umekuja utandawazi watu wamezirudia, lakini jamii iwe makini isiige kila kitu," anasema.

"Tulifanya operesheni hiyo kwa muda wa mwezi mmoja mitaani na majumbani na kuchana nguo zote fupi na za kubana ili kurudisha maadili mema ndani ya jamii na heshima ya Mtanzania," anasema Ligora.

"Waziri Mkuu wa wakati huo, Rashid Kawawa, maarufu Simba wa Vita, alitupongeza kwa kufanikisha kazi hiyo ambayo yalikuwa na maelekezo ya Baba wa Taifa kupitia kwake," anasema.

---

## Naikumbuka siku niliyofurahi hadi nikalia, kila kaya mtaani ilikesha

**INATOKA UK.13**

kuwapo na waliishi katika mazingira magumu gizani, familia zenye uwezo ndizo ziliwasha taa za karabai na chemli, viongozi na wenye uwezo walitumia umeme wa jenereta.

Anaungana na Luteni Kanali Makelelea, kuwa ni mwaka huo mvua kubwa zilinyesha mfululizo kila siku, ambayo ilileta neema ya kupatikana vitoweo vingi vya samaki aina nembe, kamongo, kambale, ningu, sato gogogo na wengine wengi kutoka mitoni na Ziwa Victoria, akisema dagaa na sangara hawakuwapo wakati huo.

### MIUNDOMBINU UCHUMI

Bibi Justa anasema kulikuwapo shule moja ya jamii ya Waasia iliyoitwa Chopra, ambayo sasa ndiyo Mwanza Sekondari na hapakuwapo umeme. Waliishi kwa kutumia chemli na vibatari, huku nyumba nyingi zikianguka na mvua kwa sababu zilijengwa kwa udongo bila ya kuwa na msingi wa mawe.

Pia anataja maeneo mengi yalijaa maji yakawa hayapitiki na madaraja yalikatika, lakini maisha yalikuwa bora, hapakuwapo njaa, walipata samaki kirahisi kwenye majaruba walipolima mpunga na mazao mengine ya chakula.

Mkongwe Justa anasema baada ya Mwalimu Nyerere kushika nchi, alitangaza kuondoa adui; ujinga, maradhi na umaskini na kutetea wanyonge, kupitia Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea.





# Mikoa Pwani, Kanda ya Ziwa yaongoza ugonjwa selimundu

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

KILA mwaka watoto 11,000 huzaliwa na ugonjwa wa selimundu (Sickle Cell) huku mikoa ya Kanda ya Ziwa na Pwani ikiongoza.

Wataalamu wa afya na wadau wametakiwa kushirikiana kutoa elimu kwa jamii ili kukabiliana na hali hiyo.

Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa anayeshughulikia Afya, Dk. Grace Magembe, aliyasema hayo jana alipokuwa akipokea ripoti ya Tanzania Sickle Cell Disease Alliance (TANSCDA), iliyoeleza jinsi ilivyotoa elimu ya upimaji na jinsi ya kujikinga na ugonjwa wa selimundu katika shule na vyuo nchini.

Alisema kwa upande wa mikoa ya Kanda ya Ziwa na Pwani, tatizo hilo ni kubwa na kuwataka wataalamu wa afya kuhakikisha kunakuwa na mashine zitakazotambua mgonjwa mwenye vinasaba vya selimundu mapema ili kusaidia kupata matibabu kwa haraka.

"Kwenye masuala ya kuangalia afya ya jamii hatuangalii gharama ndio maana kuna gharama serikali huwa inazibeba sababu suala hili linagusa afya ya kila Mtanzania," alisema. Alitoa wito kwa jamii kutowanyanyapaa wagonjwa wa selimundu na kuwataka wataalamu na wadau kutumia njia rahisi ya mawasiliano ambayo itatoa ujumbe na elimu kwa jamii ya ungonjwa wa selimundu.

"Ni vizuri pia kuwapatia elimu viongozi wetu wa dini na kimila wa kijua elimu kuhusu ugonjwa wa selimundu ni vizuri itasaidia wao kutoa sababu asilimia kubwa ndoa zinafungwa kanisani na msikitini wakijua hii elimu itatusaidia kuitoa kwa jamii," alisisitiza.

Naye Mtendaji Mkuu, TANSCDA, Dk. Deogratias Soka, alishukuru serikali na kuiomba kuendelea kuiunga mkono taasisi hiyo ili kuendelea kutoa elimu kwa jamii.




Baadhi ya wanafunzi wa shule mbalimbali za Jiji la Dodoma, wakifurahia huku wakiwa na picha ya Rais wa Kwanza wa Tanzania, Mwalimu Julius Nyerere (kushoto) na Rais Samia Suluhu Hassan, wakati wa kilele cha maadhimisho ya Miaka 60 ya Uhuru, kwenye viwanja vya Nyerere Square, jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# K/Mkuu ataka takwimu sahihi rasilimali maji

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

KATIBU Mkuu Wizara ya Maji, Mhandisi Antony Sanga, amesema kuna umuhimu mkubwa wa kuwa na takwimu sahihi za rasilimali za maji nchini.

Aidha, amewataka wataalamu kuandaa takwimu zitakazosaidia wizara kupiga hatua kwa kupanga matumizi bora ya rasilimali za maji.

Aliyasema hayo jijini hapa jana alipokuwa akifungua warsha ya kujengea uwezo wataalamu wa maji ili kutambua umuhimu wa matumizi ya takwimu, uchambuzi na tathmini katika kupanga matumizi ya rasilimali za maji kwenye Mto Nile. Alisema ni vyema wataalamu kuweka utaratibu wa kuandaa takwimu sahihi ambazo zitasaidia wizara.

Vilevile, alisema ukiwa na takwimu sahihi itakusaidia kukabiliana na mabadiliko tabianchi pale yanapotokea.

Pia alisema takwimu zitasaidia kufanya uamuzi sahihi wa kazi inayokwenda kufanyika husussani taifa likiwa katika mabadiliko ya tabianchi.

Kutokana na hayo alisema data ni kitu cha muhimu sana katika suala la utendaji kazi sekta ya maji.

Hata hivyo, aliwapongeza washiriki wa warsha hiyo huku akiwataka kusikiliza kwa makini na kwenda kuyafanyia kazi katika vituo vyao vya kazi.

Akizungumzia kuhusu suala la mvua alisema ni vyema kutumia maji ya mvua kwa ajili ya kuyahifadhi badala ya kuyaacha yapotee kizembe.

Alisema ni vyema mabwawa yakachimbwa kwa ajili ya kukusanya maji kama moja ya njia ya kukabiliana na upotevu wa maji ya mvua.

"Idadi ya washiriki ni ndogo tofauti na idadi ya wataalamu wanaofanya kazi katika Bonde la Mto Nile, wizarani na taasisi nyingine kutokana na hilo nawataka washiriki wa warsha hii kuwa makini ili kwenda kuwapa elimu na wenzao ambao hawakupata nafasi ya kuja kushiriki katika warsha hii," alisema Sanga.

Alisema kila mmoja kwa nafasi yake, anapaswa kwenda kutoa elimu ya kile walichojadili kwa wenzake ili nao wajue mikakati waliojiwekea kuhakikisha wanaboresha sekta ya maji nchini.

# CPB yakabidhi msaada wa vitimwendo

**Na Peter Mkwavila,** CHEMBA

BODI ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB), imekabidhi vitimwendo (wheel chair) vinne vyenye thamani ya Sh. milioni mbili kwa ajili ya kuwasaidia watu wenye ulemavu.

Vitimwendo hivyo vimekabidhiwa kwenye maadhimisho ya siku kimataifa ya watu wenye ulemavu yaliyofanyika wilayani Chemba mkoani Dodoma na Meneja Utawala wa bodi hiyo mkoa wa Dodoma, Amisa Shaban kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu, Dk. Anselm Moshi.

Shaban alisema katika kutambua na kuthamini mahitaji na haki za msingi za watu wenye ulemavu wameona vitimwendo hivyo vitaweza kusaidia kuwawezesha kufanya shughuli zao mbalimbali na kujitegemea kiuchumi na kuwasaidia wengine.

Alisema ni imani yake kuwa taasisi zote za serikali na zisizo za kiserikali na kidini zitaendelea kushirikiana kusaidia watu wenye ulemavu nchini ili waweze kujimudu kujiinua kiuchumi.

"Hivyo taasisi, mashirika na wadau wa maendeleo tuendelee kutoa ushirikiano katika kushughulikia masuala ya watu wenye ulemavu ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa mahitaji yao muhimu," alisema.

Aidha, alisema watu wenye ulemavu wana mahitaji mengi ya msingi zikiwano huduma za kiafya na mazingira mazuri ya kuwawezesha kuishi bila matatizo.

"Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko kama taasisi za umma imekuwa ikishirikiana mara kwa mara na jamii kwa kutoa misaada mbalimbali kulingana na mahitaji ya jamii husika kama namna ya kurejesha inachokipata kwa jamii pia kujenga uhusiano wenye manufaa kwa bodi na jamii," alisema.

Mwenyekiti wa Shirikisho la Vyama vya Watu wenye Ulemavu (SHIVYAWATA) Mkoa wa Dodoma, Omary Lubuva, akizungumza kwenye maadhimisho hayo aliziomba taasisi mbalimbali kuwaunga mkono watu wenye ulemavu ili waweze kuondokana na umaskini.

Lubuva, alisema bado watu wenye ulemavu wana uhitaji mkubwa wa kuwawezesha kukabiliana na matatizo wanayokutana nayo ikiwamo ukosefu wa elimu, huduma za kiafya na mazingira wanayoishi kutokuwa rafiki.

Kadhalika, aliziomba taasisi, mashirika ya dini na wadau wa maendeleo pamoja na serikali kuliwezesha kundi hilo katika nyanja mbalimbali ikiwamo fursa za mikopo.

Mmoja wa mnufaika aliyekabidhiwa vitimwendo hivyo Salima Mustaph (13), mkazi wa kijiji cha Jinjo, Kata ya Churuku, alisema msaada waliopewa utawawezesha familia zinazowalea kufanya shughuli zao za kujiingizia kipato kwa urahisi tofauti na ilivyokuwa awali.



# Neema yawanukia wakulima mahindi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKULIMA wa mahindi wa mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, wameanza kupata matumaini ya kuwa na soko la uhakika la mazao yao kutokana na kiwanda cha kuzalisha bidhaa mbalimbali zitokanazo na zao hilo cha East Africa Starch kuwa mbioni kukamilika.

Kiwanda hicho kinatokana na kubadili matumizi ya kilichokuwa kiwanda cha Nguo cha Mbeya (Mbeya Textile) kilichoko eneo la Songwe viwandani katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

Ofisa Utumishi wa Kiwanda hicho, Mariam Bakari, alisema jana kuwa kiwanda hicho kitakuwa kinazalisha mafuta ya kupikia yatokanayo na mahindi, chakula cha mifugo, glukozi na wanga kwa ajili ya matumizi ya binadamu na viwanda.

Alisema kiwanda hicho kitakuwa na uwezo wa kuchakata mahindi mpaka tani 90,000 kwa mwaka hali ambayo itawasaidia wakulima kupata soko la uhakika la mazao yao.

Bakari alisema kiwanda hicho kitakuwa kikubwa kuliko viwanda vyote vya Afrika Mashariki vinavyozalisha bidhaa zitokanazo na mahindi.

"Mbali na kuwahakikishia wakulima uhakika wa soko, pia kitasaidia kuongeza ajira kwa wananchi wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini. Kiwanda kitakuwa na uwezo wa kuajiri mpaka watu 300 kwa kuanzia na wataongezeka kadri mahitaji yatakavyokuwa yanaongozeka," alisema.

Mwakilishi wa Kampuni ya Export Trading Group (ETG) ambayo ni miongoni mwa wamiliki wenza, James Mariki, alisema kiwanda hicho kilianza kujengwa mwaka 2017 baada ya kubadili matumizi ya kiwanda hicho ambacho kilikuwa cha nguo.

Alisema kiwanda hicho awali kilikuwa kikizalisha nguo, lakini wakakibadili matumizi baada ya kuadimika kwa malighafi kutokana na serikali kuzuia uzalishaji wa pamba katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kwa sababu ya kusambaa kwa funza wekundu.

Mariki alisema kwa sasa kiwanda kinachelewa kukamilika kutokana na mgogoro kati yao na makandarasi ambao wanashindwa kukamilisha mradi na baadhi yao wanataka kurejea kwao India kabla ya kukamilisha kazi.

"Kwa sasa serikali imeanza kutusaidia kuwahimiza makandarasi hawa kukamilisha kazi kwa wakati. Hivi karibuni Mkuu wa Mkoa na Kamati yake ya Ulinzi na Usalama alikuja hapa na akatoa maagizo kwa makandarasi hawa na sasa tunaamini watakamilisha," alisema.

Mwishoni mwa mwezi uliopita kamati ya ulinzi na usalama ya mkoa ilifanya ziara kiwandani hapo kwa ajili ya kuangalia maendeleo na kubaini kuwa kiwanda kinachelewa kuanza kazi kwa sababu ya mgogoro uliopo.

Kutokana na hali hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, aliiagiza Idara ya Uhamiaji Mkoa wa Mbeya, kushikilia hati za kusafiria za mafundi wanaounganisha mitambo ya kiwanda mpaka watakapomaliza kazi hiyo.

Novemba 28, mwaka huu, Waziri Mkuu Majaliwa Kassim alitembelea kiwanda hicho na kumwagiza Homera kuendelea kushikilia hati za kusafiria za mafundi hao mpaka serikali itakapojiridhisha kuwa kiwanda kinaanza kufanya kazi.



Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya-WSSA), Edna Mwaigomole, akizungumza wakati wa hafla ya Maadhimisho ya Miaka 60 ya Uhuru, iliyoandaliwa na mamlaka hiyo katika chanzo cha maji cha Nzovwe, jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Kibano taasisi za serikali malimbikizo madeni ya maji

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, ametoa miezi mitatu kwa taasisi zote za serikali zinazodaiwa ankara za maji na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya-WSSA).

Mamlaka hiyo inazidai taasisi hizo zaidi ya Sh. bilioni 2.3 na Homera ameagiza kulipa fedha hizo kabla ya operesheni ya kukata maji haijazifikia.

Homera alitoa agizo hilo juzi wakati wa Mbeya-WSSA ilipokuwa inaadhimisha Miaka 60 ya Uhuru kwenye hafla maalumu iliyofanyika katika chanzo cha maji cha Nzovwe ambacho ni miongoni mwa vyanzo vikuu vinavyohudumia wananchi wa jiji la Mbeya. Alisema ikifika Februari 7, mwakani, taasisi za serikali zote ambazo zitakuwa hazijalipa madeni, zinatakiwa kusitishiwa huduma hiyo isipokuwa Magereza, Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya na Hospitali ya Rufani ya Mkoa.

Taasisi zingine zote, alisema zinatakiwa kusitishiwa huduma hiyo kwa kutumia operesheni maalumu ambayo itaundwa na vyombo mbalimbali vya dola na kwamba bila kufanya hivyo, taasisi hizo haziwezi kulipa.

Homera alisisitiza kwamba endapo taasisi hizo zitakuwa hazilipi huduma hiyo, kuna hatari mamlaka ikashindwa kujiendesha, hivyo ikafa hali ambayo itasababisha matatizo zaidi kwa wananchi.

Aliagiza mamlaka kuendelea kuwafungia wateja mita za lipa kabla kwa kuwa zitawalazimisha wateja kulipa haraka ankara zao.

Homera alisema kumekuwa na tatizo la wananchi wa kawaida kusitishiwa huduma kama hawajalipa lakini kwa taasisi za serikali inakuwa vigumu hali ambayo alisema ni makosa na wanatakiwa kurekebisha.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mbeya-WSSA, Gilbert Kayange, alisema fedha wanazozidai taasisi za serikali zikipatikana zitasaidia kupanua huduma ya majisafi na majitaka katika maeneo ya Jiji la Mbeya na Mji wa Mbalizi.

## Watoto mazingira magumu wasaidiwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATOTO 10 wanaoishi kwenye mazingira magumu katika Wilaya ya Mbeya, wamenufaika na msaada wa bima za afya ili kuwasaidia kupata matibabu wanapougua pamoja na mahitaji mbalimbali ya nyumbani.

Msaada huo ulitolewa juzi na kikundi cha Exodus Women Group kinachoongozwa na Mtendaji wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi, Elizabeth Lyombe.

Alisema kikundi hicho kiliamua kuanza kutoa misaada hiyo kutokana na kubaini kwamba watoto wengi wanaoishi kwenye mazingira magumu wanapata matatizo ya kiafya, lakini wanashindwa kutibiwa na baadhi wanakosa mahitaji muhimu.

Alisema kikundi hicho kinawasaidia zaidi watoto ambao wanalelewa kwenye familia maskini tofauti na vikundi vingine ambavyo huwa vinawasaidia watoto wanaoishi kwenye vituo vya kulelea watoto yatima.

"Tulianza mwaka jana kwa kuanza na watoto watano ambao tuliwakatia bima za afya na leo tunawakabidhi watoto 10 bima pamoja na mahitaji muhimu lakini tutaendelea kufanya hivyo ili kulisaidia kundi hili muhimu kwa taifa," alisema Lyombe.

Ofisa Ustawi wa Jamii wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Emiliana Mbise, alikishukuru kikundi hicho kwa msaada huo kuwa wako watoto wengi ambao wanaishi kwenye mazingira magumu.

Alivitaka vikundi vingine pamoja na watu wenye uwezo wa kiuchumi kuyasaidia makundi maalumu kwa maelezo kuwa misaada hiyo inasaidia kuzifariji familia hizo.



# Rais Samia Suluhu apongezwa maadhimisho miaka 60 Uhuru

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

BARAZA la Vyama vya Siasa nchini limempongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuadhimisha miaka 60 ya Uhuru wa Tanganyika huku wakiahidi kuendesha siasa za nchi kwa njia ya kistaarabu na kuzingatia misingi ya amani na utulivu.

Hayo yalisemwa jana na Mwenyekiti wa Baraza hilo, Juma Ali Khatib, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuelekea maadhimisho ya miaka 60 ya Uhuru wa Tanganyika pamoja na mkutano mkuu wa baraza hilo utakaofunguliwa na Rais Samia, Desemba 16.

Alisema wakati Watanzania wakiadhimisha uhuru wa miaka 60 yapo mafanikio mengi yamepatikana kupitia uchumi na maendeleo na demokrasia kufuatia nchi kuingia katika mfumo wa vyama vingi mwaka 1992.

Alisema baraza hilo ni taasisi iliyoanzishwa kwa mujibu wa sheria ambayo ipo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na kusimamiwa na Msajili wa Vyama vya Siasa, imefurahishwa na kazi nzuri inayofanywa na Rais Samia katika kuiongoza Tanzania kwa kuzingatia misingi ya demokrasia na utulivu wa kisiasa.

Alisema katika kipindi cha uongozi wake, Rais Samia ameahidi kufanya kazi na vyama vya siasa na kushirikiana navyo kuzipatia ufumbuzi changamoto mbalimbali zinavyovikabili vyama hivyo kwa njia ya usalama.

Alisema baraza litaendelea na majukumu yao ikiwamo kuishauri serikali njia sahihi za kuendesha siasa za kistaarabu nchini zitakazozingatia maslahi ya taifa na wananchi wake na kuepuka vurugu za kisiasa.

"Baraza la vyama vya siasa nchini tunatoa salamu zetu za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama kwa kutimiza miaka 60 ya Uhuru wa Tanganyika huku tukiahidi kuendesha harakati za kisiasa nchini kwa kuzingatia maslahi ya umma na watu wake bila ya kusababisha vurugu," alisema.

Khatib aliyataja mafanikio ya miaka 60 ya Uhuru wa Tanganyika kuwa ni pamoja na nchi kuendelea kufuata misingi iliyoachwa na rais wa kwanza wa Tanganyika na Jamhuri ya Muungano Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere ya kuwa nchi yenye uhusiano mzuri na majirani zake katika kujenga miundombinu ya mawasiliano ya usafirishaji.

Alisema Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere siku zote alikuwa akiamini Uhuru wa Tanganyika hauwezi kuwa wa kweli kama zipo nchi jirani zitakuwa zikiendelea kutawaliwa na wakoloni.

Alisema hatua hiyo iliifanya Tanzania kutumia muda mwingi ikiwamo rasilimali zake kwa ajili ya kuhakikisha mataifa ya nchi jirani ikiwamo Kusini mwa Janga la Sahara yanakuwa huru.

"Uhuru wa Tanganyika ulikuwa kichocheo kwa mataifa ya Afrika ya Mashariki kupata Uhuru kutoka kwa Muingereza, Kenya ilipata uhuru Desemba 12, mwaka 1962 na Uganda ilijikomboa mwaka 1962 Oktoba 9," alisema.

Akitoa tathmini ya vyama vya siasa nchini, alisema vinaendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria na kuishauri serikali ikiwamo msajili wa vyama vya siasa ambaye ndiye mlezi wa baraza hilo.

Aidha, alisema watahakikisha wanakuwa daraja la uhusiano na serikali kwa ajili ya kuwawakilisha wananchi ambao ndiyo wanaounda vyama vya siasa na kuona vyama vipo kwa maslahi ya taifa na sio kujenga chuki na serikali na vyombo vya dola.

Baraza la Vyama vya Siasa nchini linatarajiwa kufanya mkutano wake mkuu huko Dodoma Desemba 16 ambao utafunguliwa na Rais Samia na kufungwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi.



Maofisa wa Wakala wa Vipimo (kushoto), wakitoa elimu kuhusu matumizi sahihi ya vipimo kwa wananchi waliofika kwenye maonyesho ya wajasiriamali katika viwanja vya Maisara Zanzibar, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wahamasishwa kujitokeza maonyesho wajasiriamali

**Na Mwandishi Wetu**
ZANZIBAR

WAKAZI wa Zanzibar wamehimizwa kujitokeza kwa wingi kwenye maonyesho ya wajasiriamali kawenye viwanja vya Maisara kwa lengo la kupata elimu kuhusu matumizi sahihi ya vipimo.

Elimu ya vipimo inatolewa kwa ushirikiano wa taasisi mbili ambazo ni Wakala wa Vipimo Tanzania Bara (WMA) na Wakala wa Vipimo Zanzibar (ZAWEMA), kwenye maonyesho hayo.

Akizungumza na gazeti hili katika maonyesho yanayoendelea katika viwanya vya Maisala, Mkurugenzi wa Vipimo Zanzibar, Mohammed Mwalim Simai, alisema kwa mujibu wa Sheria ya Vipimo Wakala wa Vipimo, ndiyo taasisi pekee inayosimamia matumizi sahihi ya vipimo.

Alisema wakala huo unapaswa kuhakikisha kuwa vipimo vinavyotumika katika biashara viko sahihi, ili kuwalinda walaji na watumiaji wote. Aliwataka wananchi watembelee banda la wakala wa vipimo kupata ufahamu wa majukumu yanayotekelezwa na taasisi hiyo ikiwa ni pamoja na kufanya uhakiki wa vipimo mbalimbali.

Alisema vipimo hivyo ni kama mizani inayotumika kwenye maduka ya kuuzia nyama na bidhaa mbalimbali za majumbani, kutoa ushauri wa kitaalamu kwa watumiaji wa vipimo, kudhibiti vinavyotumika na vinavyopaswa kutumika katika biashara.

Naye Meneja wa Wakala wa Vipimo Kitengo cha Bandari Tanzania Bara, Peter Chuwa, alisema WMA inasimamia usahihi wa kiasi cha mafuta yanayoingia nchini kwa njia ya meli ili kuhakikisha kiasi cha mafuta kilichoagizwa na serikali kinapokelewa kikiwa sahihi.

Alisema wanafanya pia uhakiki katika flow meters zinazotumika kupokelea mafuta ambao uhakiki wake hufanyika kila baada ya miezi 12 ili kujiridhisha usahihi wake. Vilevile, alisema wakala wa vipimo inahakiki matangi makubwa yanayotumika kuhifadhia mafuta, uhakiki wa matangi ya malori yanayotumika kusafirisha mafuta ambayo pia huhakikiwa mara moja kila baada ya miezi 12.

Alisema uhakiki hufanyika kwenye vituo vya kujazia mafuta kwa kuhakiki pampu zinazotumika kujaza mafuta kwenye vituo vyote vya kuuzia mafuta, pampu zikihakikiwa na kuwa sahihi huwekewa alama maalumu ya utambuzi. Alisema alama hiyo ni stika maalumu inayoonyesha pampu hiyo kuwa imehakikiwa na hufanyika kwenye visima vya kuhifadhia mafuta ardhini (Underground tanks), mara moja kila baada ya miaka mitano.

Alisema WMA ilitembelea wajasiriamali mbalimbali kwenye maonyesho ya bidhaa za Tanzania na kuangalia zinazozalishwa na kufungaswa na wajasiriamali wa ndani.

Alisema baadhi ya wazalishaji wa bidhaa hizo wamefungasha vizuri bidhaa zao na kuweka alama za vipimo kwa usahihi na kwamba wajasiriamali ambao wamefungasha bidhaa bila kuzingatia matumizi sahihi ya vipimo, wamepatiwa elimu ya namna bora ya kufungasha bidhaa.

Alisema pia wameelimishwa namna sahihi ya kuandika alama za vipimo kwenye bidhaa zao kwa lengo la kuongeza thamani wanazozalisha ili ziweze kushindana kitaifa na kimataifa.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Wakala wa Vipimo Zanzibar, Mohammed Simai alisema, wakala utaendelea kutoa huduma bora kwa kuwalinda watumiaji wa vipimo kwa kuingia katika maeneo mapya ya utendaji kazi, kama inavyofanyika sasa upande wa Wakala wa Vipimo Tanzania Bara.

# Abaini chanzo uharibifu uhifadhi mazingira

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

OFISA Mtandao wa Ufuatiliaji wa Biashara ya Wanyamapori Afrika Mashariki, Dk. Allen Chad Mgaza, amesema katika ufuatiliaji uharibifu wa mazingira na maliasili wamebaini kundi kubwa la wanawake na vijana, halina uelewa, uliosababishwa na ukosefu wa elimu ya uhifadhi wa mazingira.

Aliyasema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari, katika mafunzo ya uhifadhi wa mazingira na maliasili kupitia njia ya mtandao (zoom) yaliyoandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JET).

Alisema licha ya uwapo wa kanuni na sheria za kuzuia uharibifu, uchafuzi wa mazingira na maliasili, lakini elimu inahitajika kwa jamii kuanzia ngazi ya elimu ya maandalizi.

Alisema elimu hiyo itasaidia jamii kuwa na uelewa wa utunzaji wa mazingira na uhifadhi wa maliasili na kutasaidia kulinda mazingira ambayo yameshaathiriwa kutokana na shughuli mbalimbali za kibinadamu.

"Uoto wetu wa asili umeanza kupotea kutokana na uchafuzi na uharibifu wa mazingira na maliasili hivyo ni vyema kudhibiti hali hiyo kwa kutoa elimu," alisema.

Alisema kutokana na uharibifu huo ikiwamo kuvamia maeneo ya wanyamapori na huduma za kijamii kumesababisha baadhi ya wanyamapori kuvamia makazi ya wananchi.

Alisema kinachojitokeza baada ya wahalifu kufanya uhalifu kwa wanyama au kuteketeza misitu, wanyama hutoroka katika makaazi yao ya asili na hupeleka jamii kushtakiwa na maofisa wa uhifadhi kutokana na kushambuliwa kwa wanyama hao.

Naye Mwenyekiti wa JET, Dk. Ellen Outara, alisema waandishi wa habari wana nafasi kubwa katika kutoa elimu ya uhifadhi wa mazingira hivyo ni vyema kutumia taaluma yao hiyo.

Alisema pia wanawake na vijana wanapaswa kushirikishwa katika ulinzi na uhifadhi wa mazingira na maliasili kwa maendeleo, endelevu ya taifa.

Kwa upande wao washiriki wa mafunzo hayo, walisema kuwa watayafanyia kazi mafunzo hayo kwa kutoa elimu kupitia taaluma yao ili Tanzania kuwa na mazingira mazuri yenye uoto wake wa asili na kuitaka JET kuendelea kuwajengea uwezo kuhusu masuala mbalimbali ya mazingira.

# Prof. Mkumbo ataka utu wa binadamu kuheshimiwa

**Na Yasmine Protace**

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo, amesema masuala ambayo yanaondoa utu wa binadamu hayatakiwi kufumbiwa macho kwa kuwa yanamwathiri zaidi mwanamke na kurudisha nyuma harakati za maendeleo kiuchumi.

Kitila aliyasema hayo kwenye maadhimisho ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia yaliyoandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), jijini Dar es Salaam na kushirikisha wadau mbalimbali kutoka ndani na nje ya nchi.

Alisema upo uhusiano kati ya ukuaji shughuli za kiuchumi ikiwamo biashara na wanawake, na kwamba nchi zinazofanya vizuri kiuchumi duniani zimefanikiwa kupiga vita ukatili wa kijinsia na kuhakikisha kuna usawa wa kijinsia.

"Katika masuala ya uchumi wanawake ni muhimu, kwa sababu wanawake asilimia 90 ya pesa za biashara wanazozipata zinarudi nyumbani na kutumika katika kulipia ada, kodi ya nyumba pamoja na matumizi ya chakula. Na pia zinaongeza mzunguko wa uchumi wa taifa," alisema Prof Mkumbo.

"Ulaya wanazingatia sana usawa wa kijinsia na kuna wanawake ni wengi katika uongozi. Tunahitaji kubadilika nchi zinazoendelea."

Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP, Lilian Liundi, alisema kuna haja ya kuwapo shule za awali maeneo ya soko kwa sababu wafanyabiashara walio wengi sokoni ni wanawake ambao hufanya biashara kutwa nzima na watoto wao maeneo hayo.

"Tunahitaji kuwaweka wanawake katika mazingira mazuri na watoto. Utakuta sokoni watoto wanarandaranda kwa sababu hawana pa kucheza au kujifunza, tunashauri masoko yawe na maeneo maalumu kwa ajili ya watoto hawa, tusiwaache wakiwa wanazurura sokoni wakati mama yake anatimiza wajibu wa kutafuta kipato cha familia," alisema Lilian.

Alisema TGNP imejikita katika kufanya tathmini ya utengwaji rasilimali fedha kwa ajili ya utelelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA).

Lilian aliongeza kwamba, kwa pamoja wanasherehekea hatua za serikali na wadau zilizofikiwa katika utekelezaji wa MTAKUWWA, kupitia utengwaji wa rasilimali fedha, kujadili namna ya kutatua changamoto zilizopo na kuweka mikakati ya kutokomeza ukatili wa kijinsia nchini.

Alisema mpango wa MTAKUWWA mwaka 2017/2018 na 2021/22, wenye kulenga kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto kwa asilimia 50 ifikapo 2022, umebainisha maeneo mahususi nane ya utekelezaji, ikiwamo kuimarisha uchumi wa kaya.

Pia, alisema mkakati ni kuangalia mila na desturi, mazingira salama katika maeneo ya umma, malezi, msaada kwa familia na mahusiano, utekelezaji na usimamizi wa sharia, utoaji wa huduma kwa waathirika wa ukatili, mazingira salama shuleni, stadi za maisha, uratibu, ufuatiliaji na tathmini.

Alisema afua zilizobainishwa katika maeneo hayo, zinaziba mianya inayochochea kushamiri kwa vitendo vya ukatili katika jamii kutokana na serikali kushirikiana na AZAKI na wadau wa maendeleo.

Mkuu wa Global Health Canada, Hellen Fytche, alisema usawa uwepo katika masuala ya kijinsia kwa wanawake, ili kuondoa ukandamizaji, akisema mwaka 2017 serikali ya nchi hiyo ilianza kuwawezesha wanawake na wasichana.




Mkurugenzi wa Mawasiliano na Uhusiano Vodacom Tanzania PLC, Rosalynn Mworia (wa pili kushoto), akichangia mada kwenye kongamano la siku ya mtoto njiti kuhusu marekebisho ya muda wa nyongeza wa likizo kwa wazazi ili kupata fursa ya kulea mtoto aliyezaliwa njiti, jijini Dar es Salaam juzi. Kampuni hiyo kwa sasa inatoa likizo ya uzazi ya miezi minne kwa wazazi wote wawili wanaopata mtoto. Wengine ni Msimamizi wa wodi ya watoto wanaopata huduma ya Kangaruu Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Sista Cleopatra Mtei (kushoto), mama aliyejifungua mtoto njiti, Nikita Mandan na mwongoza mada, Innocent Mungy. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Jokate ataka ushirikiano vita ukatili kijinsia

**Na Sabato Kasika**

MKUU wa Wilaya ya Temeke mkoani Dar es Salaam, Jokate Mwegelo, amewataka wananchi kushirikiana na serikali katika vita dhidi ya ukatili wa kijinsia, ili kukomesha vitendo hivyo kwenye jamii.

Alisema kila mtu anatakiwa kufanya sehemu yake kukomesha vitendo hivyo, ikiwamo kutoa taarifa za vitendo hivyo badala ya kuiachia serikali na asasi za kiraia zinazopambana na ukatili wa kijinsia.

Alisema hayo katika uzinduzi wa kampeni ya 'Safari Salama kwa Wasichana na Wanafunzi Bila Rushwa ya Ngono Inawezekana' zilizofanyika kwenye viwanja vya Zakhiem Mbagala jijini Dar es Salaam juzi.

Katika uzinduzi huo ulioandaliwa na Shirika la Wanawake Katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI), mkuu wa wilaya aliwakilishwa na Meneja Masoko wa wilaya Doto Killangi.

"Ukatili wa kijinsia si jambo la kufumbia macho, kila mmoja afanye sehemu yake kukomesha vitendo hivyo, ili watoto wote na wanawake waweze kufikia ndoto zao," alisema. Alisema kuna ukatili wa aina nyingi ukiwamo wa ngono ambao watoto wamekuwa wakifanyiwa katika jamii, na kwamba ni vyema jamii ikashiriki kikamilifu katika vita ya kukomesha vitendo hivyo.

Mkurugenzi wa WAJIKI, Janeth Mawinza, alisema shirika hilo lililokuwa katika wilaya mbili za Kinondoni na Ilala, sasa limezindua kampeni ya kupinga ukatili wa kijinsia Temeke likiwa limebakiza Kigamboni na Ubungo.

"Shirika linaendesha shughuli zake kwenye jamii, vikundi na shuleni ili kufikia walengwa kwa urahisi kwa kutumia mbinu ya mlango kwa mlango kwa ajili ya kupinga rushwa ya ngono," alisema Mawinza. Alifafanua kuwa shirika hilo limekuwa likifanya kampeni kwa madereva wa daladala, bajaji na bodaboda, kwa kuwa wao ni kiungo muhimu katika kuvunja rushwa kwa kutumia vyombo vya usafiri.

Alisema, lengo la kampeni hiyo ni kuhakikisha rushwa ya ngono inatokomezwa katika jamii ili wasichana na wanafunzi waweze kusafiri salama hatimaye watimize malengo yao ya kielimu na maisha.

"WAJIKI kwa ufadhili wa Women Tanzania Trust Fund (WFT), itahakikisha inaendelea kupanua shughuli zake nchini ili kuwajengea uwezo wanaume kushiriki kupinga ukatili wa kijinsia,"alisema.

Mwakilishi wa TAKUKURU wa wilaya hiyo, Esther Mkokota, aliwataka madereva kutambua kuwa wana nafasi kubwa ya kusaidia wasichana kutimiza ndoto zao kwa kutowarubuni.

"Ungeni mkono juhudi za serikali za kupambana na vitendo hivyo kwa kutowarubuni kwa kutimia lifti zenu, rushwa ni kosa na pia ukatili wowote ni kosa, hivyo epukeni makosa hayo," alisema Mkokota.

## NIT kutoa wahitimu vigezo vya kimataifa

**Na Mwandishi Wetu**

Wakati Chuo cha Taifa Cha Usafirishaji (NIT) kikiadhimisha kongamano la nane la wanaalumni, uongozi umesema chuo kinaendelea kufanya juhudi za dhati ili kuendelea kutoa wahitimu wenye vigezo vya kimataifa.

Akizungumza katika kongamano hilo lililofanyika katika Kampasi Kuu ya chuo hicho Mabibo, Dar es Salaam jana, Mkuu wa NIT, Profesa Zacharia Mganilwa, alisema kuwa Taasisi yao ipo kwenye mipango mikubwa itakayoweza kuzalisha wahitimu wenye viwango vitakavyowawezesha kufanya kazi kwenye miradi mikubwa iliyoanzishwa na serikali katika sekta ya usafirishaji.

"Tumeona kwa miaka ya hivi karibuni serikali imeweza kuanzisha miradi mikubwa kama vile reli ya kisasa (SGR), mradi wa umeme wa Julius Nyerere, bomba la mafuta kutoka Hoima nchini Uganda hadi Tanga na kuimarishwa kwa Shirika la Ndege Tanzania (ATCL). Kutokana na miradi hii mikubwa ya kitaifa haitahitaji kuchukua wafanyakazi kutoka nje ya nchi," Prof. Mganilwa alisema.

Alisema NIT inalazimika kufanya kazi kwa bidii ili kuhakikisha ubora wa taasisi katika ufundishaji na utafiti unaendelea kuwa imara.

Kabla ya kutolewa kwa tuzo kwa wanafunzi bora, Prof. Mganilwa liwapongeza wahadhiri wote, wakufunzi na wafanyakazi wengine wote, kwa kufanya juhudi kubwa kwa kutoa elimu bora na mafunzo yaliyotukuka na kuwafanya wahitimu hawa kumaliza masomo yao vyema.

Alisema serikali imeweka mikakati mikubwa ili kuifanya Tanzania kuwa taifa lenye uchumi mkubwa kupitia viwanda na moja ya njia ya kufikia lengo hilo ni kwa chuo kutengeneza wahitimu waliobobea katika sekta hiyo.

"Sekta ya usafirishaji inatajwa kuwa ndiyo mishipa katika kukuza uchumi wa nchi, hivyo kutokana na umuhimu huo chuo kina mikakati madhubuti kuhakikisha kinakidhi mahitaji ya rasilimali watu katika maeneo yote ya barabara, reli, maji, anga ili kufikia mapinduzi haya ya kiuchumi," alisema.

Aliwapongeza wanafunzi bora kwa mafanikio makubwa waliyoyapata ambayo hayangewezekana bila msaada wa wazazi, walezi, wadhamini ama marafiki.

Mwenyekiti wa NIT Alumni alisema kuwa dhamira kuu ya kongamano hilo ni kuhamasisha wanachuo waliosoma na wanajumuia wa NIT wenye mapenzi mema kuendelea kutoa msaada wa hali na mali kwa chuo.

HABARI PICHA

# SHEREHE ZA MAADHIMISHO YA MIAKA 60 YA UHURU WA TANZANIA BARA



Rais Samia Suluhu Hassan akisalimiana na Rais wa Rwanda, Paul Kagame, baada ya kuwasili katika Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam jana, katika maadhimisho ya miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara. **PICHA ZOTE: IKULU**



Rais Samia Suluhu Hassan, akikagua gwaride la vikosi vya ulinzi na usalama wakati wa maadhimisho hayo.




Rais Samia Suluhu Hassan, akizungumza wakati akiwasalimia na kuwapongeza Watanzania kwa kutimiza miaka 60 ya uhuru wa Tanzania Bara.



Sehemu ya umati uliohudhuria maadhimisho hayo.



Vijana wa halaiki wakionyesha umahiri wao katika mchezo wa sarakasi, wakati wa maadhimisho hayo.



Vikosi mbalimbali vya JWTZ vikipita kikakamavu mbele ya Amiri Jeshi Mkuu, Rais Samia Suluhu Hassan (hayupo pichani), katika maadhimisho ya miaka 60 ya uhuru wa Tanzania Bara.

# WAZIRI GEKUL ATOA NENO MASHINDANO YA SAMIA

**Na Saada Akida**

NAIBU Waziri wa Sanaa, Utamaduni na Michezo, Pauline Gekul, amewataka viongozi wa vyama na mashirikisho ya michezo husika kujitokeza katika viwanja kushuhudia vipaji na kupata timu ya taifa imara kwa hapo baadaye.

**Akizungumza na gazeti hili jijini jana katika upangaji wa makundi ya mashindano ya Samia Taifa Cup, Gekul alisema lengo kubwa la mashindano hayo ni kuibua vijana wenye vipaji ambao hawajapata nafasi ya kuonekana.**

Alisema katika mashindano hayo yanatoa fursa kwa vijana kuonekana na kuwataka viongozi wa klabu, timu, vyama na mashirikisho ya michezo kuhudhuria viwanjani kwa lengo la kupata wachezaji wenye vipaji.

"Haya mashindano ni muhimu kama taifa, kwa sababu yanatoa fursa kwa vijana wetu wenye uwezo na kiwango kizuri cha mchezo husika ambao wako nchini kuonekana na hapo baadaye kuisaidia timu za taifa," alisema Pauline.

Mashindano ya Samia Taifa Cup yakishirikisha michezo mitatu ikiwamo riadha, netiboli na soka kwa wanawake na wanaume yanaanza kutimua vumbi kuanzia rasmi leo Ijumaa na kumalizika Desemba 16, mwaka huu.

Viwanja vitakavyotumikia katika mashindano hayo ni Uwanja wa Benjamini Mkapa, Uhuru na JK uliopo Kidongo Chekundu jijini Dar es Salaam.

Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Michezo wa Wizara hiyo, Yusuph Singo, alisema maandalizi yamekamilika na tayari mikoa 26 imethibitisha kushiriki mashindano hayo ikiwamo Tanzania Bara na Visiwani Zanzibar.

Makundi ambayo yatacheza michuano hiyo kwa upande wa soka la wanawake ni: Kundi A: Iringa, Dar es Salaam, Tanga na Singida, Kundi B: Mwanza, Pwani, Mara na Morogoro.

Kundi C: Kusini Unguja, Dodoma, Kaskazini Unguja na Rukwa, Kundi D: Katavi, Mjini Magharibi Unguja, Arusha na Njombe.

Makundi mengine ya soka upande wa wanaume, Kundi A: Njombe, Rukwa na Mara, Kundi B: Kaskazini Pemba, Dar Es Salaam na Pwani na Kundi C: Kaskazini Unguja, Katavi na Songwe.

Kundi D: Tabora, Mjini Magharibi Unguja na Tanga, Kundi E: Mtwara, Kaskazini Unguja na Kigoma, Kundi F ni Dodoma, Morogoro na Arusha.

Makundi katika mchezo wa Netiboli ni sita ambayo Kundi A: Pwani, Geita, Njombe na Mwanza, Kundi B: Mbeya, Kigoma, Mtwara, Rukwa na Kundi C: Morogoro, Ruvuma, Tabora na Kaskazini Unguja.

Kundi D: Simiyu, Songwe, Arusha na Iringa, Kundi E: Kaskazini Unguja, Tanga, Magharibi Unguja na Dar es Salaam na Kundi F: Dodoma, Lindi, Kagera na Kaskazini Pemba.




Mshindi wa Sportpesa Jackpot bonus, Jamali Saidi Lilomba (34), kutoka Mtwara-Nanyamba akishikilia mfano wa hundi ya shilingi 10,162,547 baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 12 kati ya 13 kwenye Jackpot ya wiki iliyopita. Jackpot ya wiki hii inayoshindaniwa ni Sh. 761,374,640. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Simba Queens kusajili wachezaji wawili*

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Simba Queens umesema uko kwenye hatua za mwisho kuwapata warithi wa nyota wao wawili Flavine Mawete na Ruth Kipoyi kwa lengo la kuimarisha kikosi cha timu hiyo kwa msimu mpya wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania Bara.

Mawete raia wa DR Congo ameondoka Simba Queens na kwenda kujiunga na klabu ya A.B.B Fomget na Kipoyi kujiunga na klabu ya Algspor Kulubu, inayoshiriki Ligi Kuu ya Wanawake nchini Uturuki.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Meneja wa Simba, Selemani Makanya alisema baada ya wawili hawa kuelekea nchini Uturuki kwa ajili ya kutafuta maisha mapya ya mpira sasa wako katika hatua za mwisho kuziba nafasi za nyota huyo.

Alisema wana imani dirisha dogo likifunguliwa watakuwa tayari wamepata watu sahihi wa kuziba nafasi za nyota hao na kuhakikisha wanasaidia timu yao kufikia malengo yao msimu huu.

"Licha ya msimu huu tumekuwa na mabadiliko ya benchi la ufundi kwa kuleta Kocha mpya, Sebastian Nkoma ambaye anaendelea vizuri na maandalizi ya timu hiyo kwa ajili ya kuleta ushindani na kufikia malengo yao," alisema Selemani.

## Prisons yaipiga mkwara Yanga

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kuchapwa bao 1-0 dhidi ya Polisi Tanzania Desemba 4 kwenye Uwanja wa Ushirika mjini Moshi, timu ya Prisons imesema kuwa nguvu zake sasa inaelekeza kwenye mechi ya Kombe la FA dhidi ya Kitayosce pamoja na Yanga.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Jackson Mwafulango, amesema kuwa kikosi chao kimeanza mazoezi kujiandaa na michezo hiyo miwili muhimu ambayo wamejiandaa kushinda.

"Tumerudi Sumbawanga kutoka Moshi ambako tulipoteza kwa bao 1-0 dhidi ya Polisi Tanzania kwa bao la dakika za mwisho kabisa, tumeanza mazoezi kwa ajili ya mechi zetu mbili zinazotukabili. Tutaanza kucheza na Kitayosce ya Tabora kwenye Kombe la FA Desemba 15, halafu baada ya hapo tutakabiliana na Yanga Desemba 19 na hizi mechi zote mbili tunazichukulia kwa uzito mkubwa, tunachotaka kwanza tusonge mbele kwenye michuano ya FA kwa sababu lengo letu ni kufika fainali na hata kulichukua, pili kuifunga Yanga ili tukae vizuri kwenye msimamo wa ligi na uwezo huo tunao," alisema Ofisa Habari huyo.

## Ogopa Sokoine Mbeya kwa kujifunga

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Ligi Kuu Tanzania Bara imeingia kwenye raundi ya nane, wachezaji watatu wamejifunga mwenyewe, huku uwanja wa Sokoine mjini Mbeya, uliongoza kwa mabao ya kujifunga.

Mabao mawili ya kujifunga, wamefungwa kwenye Uwanja wa Sokoine mjini Mbeya, huku moja likifungwa kwenye Uwanja wa Nelson Mandela mjini Sumbawanga.

Timu za jijini Mbeya, Mbeya Kwanza na Mbeya City, zimenufaika na mabao yote matatu ya kujifunga mpaka sasa kwenye Ligi Kuu.

Mbeya Kwanza ndiyo inaonekana kunufaika zaidi, kwani mabao mawili ya kujifunga msimu huu, imeihusisha timu hiyo wapinzani wao wakijifunga.

Yahaya Mbegu wa Polisi Tanzania aliuweka mwenyewe mpira wavuni, wakati timu yake ilipocheza dhidi ya Mbeya Kwanza kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya, mechi iliyoisha kwa sare ya mabao 2-2, mechi iliyochezwa Novemba Mosi mwaka huu.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**RAMSEY HUYO EVERTON**

KIUNGO wa kati wa Juventus na Wales, Aaron Ramsey, 30, huenda akajiunga na klabu ya Everton Januari. ***(Calciomercato)***

**WACHEZAJI HAWAFURAHI**

WACHEZAJI wa Chelsea hawafurahii kwanini klabu hiyo haijamwongezea mkataba Cesar Azpilicueta, 32, huku Atletico Madrid ikiwa na nia ya kumsajili mlinzi huyo wa Hispania. ***(Eurosport)***

**MARCELO KUONDOKA**

MLINZI wa kushoto wa Real Madrid, Marcelo, 33, anatarajiwa kukamilisha mkataba wake baada ya kuichezea klabu hiyo kwa miaka 15 wakati itakapokamilika mwaka ujao na kujiunga na klabu ya Fluminense nchini Brazil. ***(Mirror)***

**WIJNALDUM ATAKIWA ARSENAL**

KLABU ya PSG iko tayari kuchukua maombi ya mkopo kwa aliyekuwa kiungo wa kati wa Liverpool, Georghinio Wijnaldum, 31, katika dirisha la uhamisho la Januari. Mchezaji huyo raia wa Uholanzi yuko tayari kurudi katika Ligi Kuu ya England na Arsenal wameonyesha nia ya kumtaka. ***(Sky Sports)***

**YAMTAKA GEORGHINIO**

KLABU ya Newcastle United pia imeonyesha nia ya kutaka kumsajili Georghinio Wijnaldum na huenda ikawasilisha ombi la kumsajili raia huyo wa Uholanzi katika dirisha la uamisho la Januari. (Marca)

**ELNENY ATAKIWA NEWCASTLE**

NEWCASTLE inawania kuwasajili wachezaji watano katika dirisha la uhamisho la Januari, ambao ni pamoja na kiungo wa kati wa Misri, Mohammed Elneny, 29. ***(Mirror)***

**DIGNE KUUZWA**

KOCHA wa Everton, Rafael Benitez alimwacha nje Lucas Digne, 28, katika ushindi dhidi ya Arsenal kutokana na mgogoro na sasa beki huyo wa kushoto wa Ufaransa huenda akauzwa mnamo Januari. ***(The Athletic)***

**CAVANI KUBAKI**

KOCHA wa klabu ya Manchester United, Ralf Rangnick amesema anatumaini atashirikiana na mshambuliaji wa Uruguay, Edinson Cavani, 34, katika kipindi kilichosalia cha msimu. Mchezaji huyo amehusishwa na uvumi wa kuondoka Old Trafford. ***(Manchester United)***

**MOYES KUSAJILI BEKI**

KOCHA wa klabu ya West Ham, David Moyes anataka kusajili beki Januari baada ya wachezaji, Kurt Zouma na Angelo Ogbonna kuwa majeruhi. ***(Mail)***

**KULUSEVSKI ANUKIA ARSENAL**

ARSENAL inakaribia kufikia makubaliano na mchezaji wa Juventus na Uswisi, Dejan Kulusevski, 21. ***(La Repubblica, via Sun)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# TUCHEL ATAKA ZAIDI KWA WACHEZAJI

**Asema hajapendezwa kuruhusu mabao matatu ndani ya wiki moja huku...**

**MOSCOW,** Misri

KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel amesema anataka zaidi kutoka kwa wachezaji wake baada ya kuona timu yake ikipoteza nafasi ya kupaa kileleni kwenye Kundi H baada ya sare ya 3-3 dhidi ya Zenit kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, Jumatano.

**Blues hao walikuwa wametoka nyuma kwa mabao 2-1 hadi mapumziko wakiwa mbele kwa mabao 3-2 na Magomed Ozdoev akasawazisha na kuwanyima ushindi.**

Hiyo ilikuwa na maana kwamba, Juventus walichukua uongozi wa kundi baada ya kuwafunga 1-0.

Mabao mawili ya Timo Werner na Romelu Lukaku ya kwanza tangu arejee kutoka kwenye majeraha yalionekana kuwatosha Chelsea kabla ya Ozdoev kusawazisha dakika ya 94 kwenye Uwanja wa Gazprom Arena.

Kikosi cha Tuchel kililazimika kushika nafasi ya pili katika Kundi H, na Mjerumani huyo alikasirishwa na kufungwa mabao matatu katika mchezo kwa mara ya pili ndani ya wiki moja, baada ya kushuhudia Chelsea ikifungwa 3-2 na West Ham Jumamosi.

"Kama wewe ni kocha wa Chelsea na unaruhusu mabao sita katika mechi mbili, mara nne tumetoa uongozi ugenini, matarajio yangu ya kuzungumzia kiwango cha wachezaji binafsi si ya juu sana," alisema akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo.

"Hatuwezi kuwa na furaha leo (juzi) au dhidi ya West Ham. Hakuna anayeweza kuwa na furaha.

Chelsea walianza vyema, kwa kupata bao la kuongoza katika dakika ya pili tu kupitia kwa Werner, lakini waliwekwa kwenye presha kubwa na Zenit kwa kipindi kirefu cha kipindi cha kwanza, huku wenyeji wakifunga mara mbili kutokana na mashuti tisa ambayo waliruhusiwa katika dakika 45 za mwanzo.

"Nadhani tulikuwa na dakika 15 nzuri za kwanza lakini tuliacha kufanya mambo tuliyofanya," Tuchel aliongeza.

"Nilikuwa na hisia, na haya ni maoni yangu, kwamba tulisahau kwa nini tulikuwa timu bora zaidi. Na mara hii ikishuka, mara tunapoanza kusimamia matokeo, tunaadhibiwa."

HABARI MICHEZO

MECHI KALI
HOME
BRENTFORD
2.10 | 3.36 | 3.51
WATFORD
AWAY
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 761



# LAPORTA ATAKA UMOJA BARCELONA

**MUNICH,** Ujerumani

RAIS wa Barcelona, Joan Laporta ametoa wito wa umoja baada ya klabu hiyo kutupwa nje kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Barca ilitolewa kwenye michuano hiyo hatua ya makundi kwa mara ya kwanza tangu msimu wa 2003-04, ikifungwa mabao 3-0 na Bayern Munich pale kwenye uwanja wa Allianz Arena, Jumatano.

Kikosi hicho kinachonolewa na kocha, Xavi kilihitaji ushindi au Benfica kufungwa na Dynamo Kiev ili kiweze kutinga hatua ya mtoano wa timu 16.

Lakini wababe hao wa LaLiga walishindwa kutamba mbele ya Bayern, ambao mabao yake yalifungwa na Thomas Muller, Leroy Sane na Jamal Musiala.

Hiyo ni mara ya nne kwa Barcelona kuondolewa katika hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa baada ya msimu wa 1997-98, 1998-99 na 2000-01, na mara ya pili kuangukia kwenye michuano ya Ligi ya Europa tangu msimu wa 2000- 2001.

Barca pia wamo katika nafasi ya saba kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, wakiwa na pointi 16 huku Laporta akishughulikia masahibu ya klabu hiyo.

"Hatujaweza kushuka kwenye vyumba vya kubadilishia nguo kuwainua wachezaji, tutazungumza na makocha kwenye ndege.

# Pele alazwa hospitali

**SAO PAULO,** Brazil

GWIJI wa soka wa Brazil, Pele amelazwa hospitali akisumbuliwa na matatizo ya uvimbe kwenye utumbo mpana.

Mshindi huyo mara tatu wa Kombe la Dunia alifanyiwa upasuaji wa kuondoa uvimbe kwenye utumbo mpana Septemba, huku hospitali ikisema wakati huo pia angehitaji kufanyiwa tiba ya kemikali.

Dakati wa Hospitali ya Sao Paulo, Albert Einstein, alisema kuwa Pele mwenye umri wa miaka 81 yuko katika hali nzuri na ataruhusiwa katika siku chache zijazo.

Hospitali pia ilisema Pele sasa "anaendelea" na matibabu yake.

Pele alisema kwenye Twitter mwezi uliopita kwamba alikuwa "mwenye afya" na "anajihisi bora kila siku" baada ya kuruhusiwa kutoka hospitalini Septemba.


Alikuwa akitibiwa hospitalini hapo tangu Agosti 31 baada ya uvimbe huo kugunduliwa katika vipimo vya kawaida.

Afya yake imekuwa ya wasiwasi katika miaka ya hivi karibuni na alifanyiwa upasuaji wa tezi dume mwaka 2015 baada ya kulazwa kwa mara ya pili ndani ya miezi sita, na alilazwa tena kwa maambukizi ya mkojo mwaka 2019.

Pele ndiye mfungaji bora wa muda wote wa Brazil akiwa amefunga mabao 77 katika mechi 92 na mmoja wa wachezaji wanne pekee waliofunga katika michuano minne ya Kombe la Dunia.







,374,640

# JACKPOT
## MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 11/12/21 | 18:00 | Peterborough vs Millwall | 3.04 | 3.19 | 2.29 |
| 02. 11/12/21 | 18:00 | Derby vs Blackpool | 2.34 | 3.14 | 2.99 |
| 03. 11/12/21 | 18:15 | Alaves vs Getafe | 2.37 | 2.94 | 3.34 |
| 04. 11/12/21 | 23:00 | Athletic Bilbao vs Sevilla FC | 2.64 | 3.09 | 2.79 |
| 05. 12/12/21 | 14:30 | Torino vs Bologna | 2.30 | 3.25 | 3.15 |
| 06. 12/12/21 | 15:00 | Lille vs Lyon | 2.50 | 3.49 | 2.65 |
| 07. 12/12/21 | 17:00 | Brighton vs Tottenham | 3.00 | 3.20 | 2.42 |
| 08. 12/12/21 | 17:00 | Metz vs Lorient | 2.35 | 3.28 | 2.99 |
| 09. 12/12/21 | 19:00 | Strasbourg vs Marseille | 2.64 | 3.34 | 2.59 |
| 10. 12/12/21 | 19:30 | Crystal Palace vs Everton | 2.27 | 3.20 | 3.25 |
| 11. 12/12/21 | 20:00 | Sassuolo vs Lazio | 2.89 | 3.49 | 2.34 |
| 12. 12/12/21 | 20:15 | Alcorcon vs FC Cartagena | 2.94 | 2.94 | 2.50 |
| 13. 12/12/21 | 20:30 | Betis vs Real Sociedad | 2.35 | 3.25 | 3.05 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### IJUMAA - 10 - DESEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 3048 | Van Yerevan vs FC Noravank | 2.61 | 3.00 | 2.61 |
| 14:30 | 3328 | Aluminium Arak vs Fajr Sepasi | 1.76 | 3.17 | 4.62 |
| 14:30 | 5072 | Naft Masjed Soleyman FC vs Zob Ahan | 2.93 | 2.79 | 2.50 |
| 14:30 | 5287 | Padideh Mashhad vs Gol Gohar | 8.48 | 3.76 | 1.40 |
| 14:30 | 5829 | MES Rafsanjan vs Teraktor Sazi | 1.80 | 3.08 | 4.53 |
| 16:00 | 2686 | Artsakh vs Urartu | 2.06 | 3.28 | 3.23 |
| 17:00 | 1484 | Delhi Dynamos FC vs Northeast United FC | 3.38 | 3.47 | 1.94 |
| 17:30 | 4859 | Lokomotiv Plovdiv vs Botev Vratsa | 1.30 | 4.63 | 8.67 |
| 18:00 | 1165 | Illichivec Mariupol vs SC Dnipro 1 | 5.97 | 4.52 | 1.41 |
| 18:30 | 4649 | U Craiova SA vs Clinceni | 1.77 | 3.14 | 5.11 |
| 19:00 | 5658 | Spartak Trnava vs Zemplin Michalovce | 1.32 | 4.81 | 7.50 |
| 20:00 | 1239 | Kocaelispor vs Erzurum BB | 2.98 | 3.03 | 2.31 |
| 20:00 | 1317 | Cremonese vs Crotone | 1.97 | 3.33 | 3.67 |
| 20:00 | 1712 | Hvidovre IF vs Sonderjyske | 2.15 | 3.47 | 2.89 |
| 20:00 | 4348 | Altay vs Hatayspor | 2.62 | 3.36 | 2.52 |
| 20:00 | 4502 | Genclerbirligi vs Denizlispor | 1.75 | 3.56 | 4.04 |
| 20:00 | 4535 | Pafos FC vs AEL Limassol | 2.43 | 3.22 | 2.87 |
| 20:00 | 4810 | Istra vs Hrvatski Dragovoljac | 1.46 | 4.15 | 5.79 |
| 20:30 | 1217 | FC Ingulets vs Desna Chernigov | 2.71 | 3.19 | 2.40 |
| 20:30 | 2772 | Jahn Regensburg vs Werder Bremen | 3.04 | 3.48 | 2.16 |
| 20:30 | 4328 | Schalke 04 vs Nurnberg | 1.98 | 3.30 | 3.69 |
| 21:00 | 3123 | ETSV Weiche vs FC Phonix Lubeck | 1.24 | 5.40 | 9.06 |
| 21:00 | 5035 | Energie Cottbus vs Berliner Dynamo | 2.10 | 3.61 | 2.89 |
| 21:30 | 3999 | Rapid Bucuresti vs Argesul Pitesti | 2.43 | 2.89 | 3.09 |
| 22:00 | 1468 | ADO Den Haag vs Jong AZ Alkmaar | 1.39 | 4.79 | 6.45 |
| 22:00 | 1777 | Roda Kerkrade vs Den Bosch | 1.39 | 4.69 | 6.64 |
| 22:00 | 2489 | FC Volendam vs Jong PSV | 1.43 | 4.67 | 5.84 |
| 22:00 | 3176 | FC Oss vs Jong Ajax | 2.83 | 3.66 | 2.18 |
| 22:00 | 3219 | NAC Breda vs Almere City | 1.91 | 3.76 | 3.37 |
| 22:00 | 3704 | Emmen vs Dordrecht | 1.20 | 6.25 | 10.75 |
| 22:00 | 4402 | FC Eindhoven vs Telstar | 2.04 | 3.52 | 3.23 |
| 22:00 | 5314 | SBV Excelsior vs Maastricht | 1.28 | 5.65 | 7.99 |
| 22:00 | 5341 | Willem II Tilburg vs Cambuur | 2.29 | 3.58 | 2.75 |
| 22:00 | 5430 | De Graafschap vs Helmond Sport | 1.28 | 5.45 | 8.17 |
| 22:00 | 5572 | VVV Venlo vs Jong Utrecht | 1.96 | 3.66 | 3.32 |
| 22:30 | 1396 | Ternana vs Benevento | 2.46 | 3.29 | 2.70 |
| 22:30 | 1614 | FC Koln vs Augsburg | 1.63 | 4.10 | 4.80 |
| 22:30 | 3213 | SC Kriens vs FC Aarau | 3.29 | 3.62 | 1.92 |
| 22:30 | 5689 | Neuchatel Xamax vs FC Thun | 2.56 | 3.29 | 2.47 |
| 22:30 | 5944 | FC Vaduz vs Yverdon-Sport FC | 1.87 | 3.61 | 3.47 |
| 22:45 | 2096 | Ayr United vs Hamilton | 2.39 | 3.18 | 2.84 |
| 22:45 | 3080 | Genoa vs Sampdoria | 3.05 | 3.20 | 2.39 |
| 22:45 | 4272 | Ballymena Utd vs Larne | 4.43 | 3.95 | 1.61 |
| 22:45 | 5404 | Charleroi vs Oostende | 1.62 | 4.04 | 4.73 |
| 23:00 | 1534 | Sporting Gijon vs Huesca | 2.27 | 3.13 | 3.13 |
| 23:00 | 3353 | CD Badajoz vs Tudelano | 1.51 | 3.61 | 6.17 |
| 23:00 | 4554 | Nantes vs Lens | 2.74 | 3.34 | 2.49 |
| 23:00 | 4955 | Mallorca vs Celta Vigo | 2.59 | 3.04 | 2.89 |
| 23:00 | 5117 | Brentford vs Watford | 2.10 | 3.36 | 3.51 |
| 23:15 | 3969 | Pacos Ferreira vs Gil Vicente | 2.67 | 3.01 | 2.72 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# AZAM YAZUNGUMZIA USAJILI WA SURE BOY

**Na Dennis Fussi**

UONGOZI wa Azam FC umetoa kauli kuhusu tetesi za kiungo wa klabu hiyo, Salum Abubakar 'Suare Boy' kuhusishwa na mpango wa kusajiliwa Yanga.

Sure Boy anayetumikia adhabu ya kusimamishwa kwa muda usiojulikana huko Azam anatajwa kuwa kwenye mpango wa kusajiliwa na Yanga wakati wa dirisha dogo la usajili, ambalo rasmi litafunguliwa Desemba 15.

Akizungumzia jambo hilo Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano ya Azam, Zakaria Thabiti amesema taarifa za mchezaji huyo kuwa mbioni kusajiliwa Yanga wanaziona kwenye mitandao ya kijamii, lakini hazijawafikia rasmi mezani kwao.

Amesema Azam haina hiyana yoyote katika suala la kumwachia mchezaji anayehitajiwa na klabu nyingine, lakini akasisitiza kufuatwa kwa taratibu za uhamisho ambazo zinatambulika duniani kote.

"Sisi hatumzuii mchezaji yeyote kusajiliwa na timu nyingine, kikubwa timu husika inahitajika kufuata taratibu za usajili," alisema Thabiti.

Sure Boy alisimamishwa na Azam mwanzoni mwa msimu huu kwa utovu wa nidhamu, sanjari na wachezaji Mudathir Yahya na Agrey Morris.




Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Pauline Gekul (katikati) akishuhudia droo ya upangaji wa makundi ya timu na ratiba ya mashindano ya Samia Taifa Cup 2021 ambayo yanatarajia kuanza leo Jijini Dar es Salaam. Kushoto Kaimu Katibu wa Baraza la Michezo la Taifa, Neema Msita, kulia ni Mkurugenzi wa Michezo, Yusu Omary Singo. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Voice Wonder aibuka upya*

**Na Sabato Kasika**

BAADA ya kimya cha muda mrefu, msanii nyota wa muziki wa kizazi kipya, Voice Wonder, ameibuka upya na sasa anajiandaa kufyatua kibao kipya akimshirikisha mwimbaji wa muziki wa dansi, Christian Bella.

Msanii huyo amesema, anarudi kwa kishindo, na kwamba, jina la kibao chake hicho kipya litajulikana akiwa tayari ameshakirekodi na kuwataka mashabiki wake kujiandaa kupokea ujio wake mpya.

"Narudi kwa kishindo, pata picha watu wenye sauti zao wanapokutana. Hapa Voice Wonder pale Christian Bella. Ndio nyimbo inayokujaa," aliandika Voice Wonder katika mtandao wa facebook.

Nyota huyo aliyewahi kutamba na kibao cha 'Nimpende Nani', amesema anaamini waliomsubiri kwa muda mrefu atakata kiu yao kwa ujio wake mpya akiwa amemshirikisha Bella.

Amesema, awali alipanga kurejea kwenye muziki mwaka 2016, lakini mambo hayakwenda vizuri, na kwamba mwaka ujao wa 2022 anarudi rasmi kendeleza kipaji chake cha kuimba muziki wa kizazi kipya.

"Sihofii kurudisha tena nafasi yangu kimuziki kwani licha ya muziki njia zote za kupitia anazijua, hivyo nina uhakika jina langu litarudi kwenye chati kama ilivyokuwa miaka ya nyuma," amesema.

Amesema, kwa muda wote ambao amekaa pembeni, amejifunza mambo mengi na kubaini kuwa kwenye muziki wa sasa idea za nyimbo nyingi zinafanana kuanzia mashairi na melody hivyo hakuna kinachomshtua.

"Kwa wale ambao hawanijui, ninawajulisha kuwa nilifanya muziki kipindi kuna watu wazito kama Inspekta Haroun, Juma Nature, Q-Chillah, Bushoke, Banana Zorro, K-Bazil na wengine wengi lakini nikapenya," amesema.

Amesema, kwa uzoefu huo, hata sasa anaweza kupenya, kwa madai kwamba muziki wa kizazi kipya kwa sasa umetawaliwa na wasanii wawili ambao ni Ali Kiba na Diamond.

Michezo

Ijumaa Desemba 10, 2021

Nipashe



Tuchel ataka zaidi kwa wachezaji UKURASA 21



Nyota wa Chelsea, Timo Werner akishangilia baada ya kufunga bao la uongozi dhidi ya Zenit St. Petersburg kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya juzi. Timu hizo zilifungana 3-3. **PICHA: MTANDAO**

# Nabi awapa walinzi majukumu Yanga SC

## ●●● Ni katika kuhakikisha wanapata ushindi mzuri dhidi ya Simba na...

**Na Saada Akida**

KUELEKEA mechi ya watani zao Simba itakayochezwa kesho Jumamosi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Kocha Mkuu wa Yanga, Nesreddine Nabi amewapa majukumu mabeki wake na kuwataka kuwa makini ili kuweza kuzuia safu ya ushambuliaji ya wapinzani wao.

**Safu ya ulinzi ya Yanga inaongozwa na mabeki wa kati, Bakari Mwamnyeto, Dickson Job, Djuma Shaban (kushoto), David Bryson (kulia) na Shomari Kibwana ambaye ni kiraka mwenye uwezo wa kucheza nafasi mbili kwa ufasaha wa hali ya juu.**

Kocha Nabi amesema kulingana na ugumu wa mechi hiyo ana imani itakuwa ya ushindani na safu ya ushambuliaji ya wapinzani wao itaingia kivingine kwa kuhakikisha wanatafuta ushindi dakika za mwazoni.

Alisema wakati kila mchezaji akipewa majukumu yake kuelekea mchezo huo pia amewasisitizia mabeki wake kuwa makini kwa kudhibiti washambuliaji wa Simba.

"Safu ya ulinzi tayari inajua majukumu yake, washambuliaji nao wanaelewa nini wanatakiwa kufanya katika mchezo huu, ambao utakuwa wa kiufundi na kimbinu zaidi kwa kila upande," alisema Nabi.

"Tunawaheshimu sana Simba, tunajua ubora na madhaifu yao, tunajiandaa kwa ajili ya kwenda kutafuta pointi muhimu katika mchezo huo," aliongeza.

Alisema kuhusu kikosi chake hasa kwenye safu ya ulinzi ana imani kila mmoja ana uwezo mkubwa na kufanya vizuri katika mchezo huo kulingana na maandalizi ambayo wanayafanya.

# Yanga yaipongeza Simba SC kuingia makundi CAF

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imeipongeza klabu ya Simba kwa kutinga hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho barani Afrika kwa kuisukumiza nje ya mashindano hayo, Red Arrows ya Zambia kwa jumla ya mabao 4-2.

Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli amesema wanawapongeza watani zao wa jadi kwa kufuzu hatua ya makundi, licha ya kwamba mechi ya marudiano walifungwa.

"Wamefuzu, hili ngoja tuwapongeze, japo wamefungwa kwenye mechi yao ya mwisho ila wamefuzu. Pamoja na kwamba wamefuzu kwa kipigo, lakini wamefuzu, tunawapongeza," alisema Bumbuli akiongeza na utani wa jadi kati ya klabu hizo mbili ambao ni wa tangu enzi na enzi.

Akizipokea pongezi hizo, Kaimu Ofisa Habari wa Simba, Ally Shatry 'Chico' alisema anazipokea kwa mikono miwili, na kwa sababu zimetolewa na Ofisa Habari wa Yanga, basi anaamini ni kutoka kwenye klabu ya Yanga na si ya mtu binafsi.

"Nipokee pongezi za Yanga, tunashukuru sana kwa niaba ya klabu ya Simba, lakini kusema sisi tumefungwa wao wameshinda si kweli, sisi tulikuwa tunacheza mechi ya kimataifa, tumefuzu, wao walikuwa wanacheza mechi ya ndani," alisema.

Simba ilitinga hatua ya makundi baada ya kuifunga Red Arrows mabao 3-0 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa Novemba 28, kabla ya kufungwa mabao 2-1 kwenye mechi ya marudiano Desemba 5 kwenye Uwanja wa Mashujaa Lusaka nchini Zambia.

Ilikuwa ni mechi ya mtoano, baada ya kuondolewa kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa na Jwaneng Galaxy ya Botswana.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P